SUPA JACKPOT
TZS. 1,151,104,636
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

# Nipashe

Alhamisi Septemba 7, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581426

www.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper

**BITEKO** aanza wadhifa mpya na maagizo 10 ndoa na watoto

UKURASA 20



**MAZUNGUMZO MAALUM**

Dk. Slaa aanika msimamo wake kuhusu dini na siasa

UKURASA 4



**KESI KINA MDEE**

Komu aihusisha NEC na wabunge 19

UKURASA 20

# Profesa mchumi adai Rais haambiwi ukweli



Prof. Haji Semboja



UKURASA 2

UKURASA WA 11




UKURASA WA 19

## WB YAIPA TANZANIA BIL. 740/- ZA KILIMO

BENKI ya Dunia (WB) imetoa mkopo wa Dola za Marekani milioni 300 (zaidi ya Sh. bilioni 746) kwa ajili ya kuboresha ...

UKURASA WA 23

## MWAKINYO, OKWIRI ULINGONI SEPTEMBA 29

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Hassan Mwakinyo, anatarajia kupanda ulingoni kupigana na Mkenya, Rayton Okwiri, katika...



**MKUTANO MIFUMO YA CHAKULA**

## Marais 7 kujadili hatima chakula Afrika

Ulega: Karibuni tuna utajiri wa mifugo milioni 70 sokoni...

Ukurasa wa 2, 8 & 19



Mshtakiwa katika kesi ya mauaji ya mkewe, Naomi Marijani, Hamis Luongo (kushoto), akijadiliana jambo na wakili wake, Zidadi Mikidadi kabla ya kuanza kusomewa maelezo ya awali ya kesi inayomkabili Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam iliyoketi katika Kituo Jumuishi cha Kutolea Haki Kinondoni, jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Wakili aiomba mahakama mteja wake apimwe akili

UKURASA 3

**MICHEZO** TAIFA STARS POINTI MOJA TU LEO ALGERIA UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Rais wa Msumbiji, Filipe Nyusi, katika Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi Afrika 2023, jijini Nairobi nchini Kenya juzi. **PICHA: IKULU**

# Profesa mchumi adai Rais haambiwi ukweli

**Na Beatrice Shayo**

MTAALAMU nguli wa masuala ya uchumi, Profesa Haji Semboja, amesema hali anayoiona katika mwenendo wa mafuta nchini ni kutokana na wasaidizi wa Rais Samia Suluhu Hassan hawamwambii ukweli.

Prof. Semboja alisema hayo wakati akitoa maoni yake kuhusu kupanda kwa bei za mafuta nchini na uhaba wa dola ya Marekani ambayo hutumika katika kununua bidhaa hiyo. Pia wadau mbalimbali, wakiwamo wachumi na waagizaji mafuta, walitoa maoni yao kuhusu jambo hilo.

Alisema Watanzania kuna haja ya kufika sehemu na kueleza ukweli kuhusu uhalisia wa upatikanaji wa dola nchini kwa kuwa nia ya Rais Samia ya kuweka nchi katika nafasi nzuri ni njema. "Hata nikisema tufanye nini katika bei ya mafuta haiwezekani nitakuwa mchawi tatizo lenyewe limegubikwa 'systems'. Mifumo ya serikali yenyewe kwa sasa haifanyi kazi vizuri kuisaidia sekta binafsi.

"Nimeenda benki, kupata dola ni shida. Kama serikali inasema kuna dola wakati mimi mwenyewe sijazipata, huyo anayasema zipo ni kwamba haipendi hii nchi. Nenda leo benki sema unataka Dola 1,000 au 2,000 huwezi kupata. Kwa nini tusiseme ukweli tuna matatizo ya dola tutafute kujua ni kwa nini? Tusidanganye kwamba zipo," alisema.

Alisema anayedai dola zipo huenda hana elimu ya kujua maana ya dola ni kitu gani na kwamba ni vyema akatafuta wataalamu wa kumsaidai ili kutatua jambo hilo badala ya kueleza uongo.

"Hivi wanataka watu waondolewe kwa nguvu madarakani? Kama mtu hawezi kumsaidia Rais Samia ni vizuri kueleza ukweli. Naweza kusema wanamfanyia Rais hujuma. hiki kinafeli na kile kinafeli wakati mama wa watu anahangaika anaweka tume za kila aina. Haya matatizo huenda kuna wengine wanafaidika.

"Matatizo yamekuwa mengi. Jambo la kwanza ni kujiuliza ni kwa nini yanatokea. Jibu ni kwa sababu hakuna sera, hakuna sheria na taratibu, hakuna taasisi na hakuna wafanyakazi katika utawala ndani ya serikali ambao wote kwa pamoja wanaendana na wakati uliopo sasa.

"Ziko sheria ambazo zinaeleza hawa watu wanapatikana vipi. Waombe watu washindanishwe wapewe hizo nafasi Watanzania wote wapo sawa hakuna haja ya kujifungia chumbani na kusema huyu anaweza na huyu hawezi tangaza nafasi zote hasa kwenye hizi taasisi zote," alisema.

Prof. Semboja alisema baada ya hayo kufanyika, ndipo Rais afanye uteuzi wa yule ambaye anaiweza nafasi hiyo. Huwezi kwenda tume ya mipango halafu walioko pale elimu zao ni tofauti. Hawawezi kukusaidia kwani watakaa kwa maslahi yao na si kwa taifa.

"Ulishawahi kusikia Airtel au Vodacom kuna matatizo? Kwa nini kwenye shirika lako la serikali linashindwa kufanya kazi yapo mashirika ambayo yangekuwa yanafanya vizuri tusingekuwa na matatizo ya dola.

"Mafuta hatuzalishi ina maana tunaagiza kutoka nje ya nchi inapotokea mabadiliko yoyote ya kifedha kwa maana ya bei, uchumi wetu utayumba. Usafirishaji wa mafuta hadi yafike Tanzania ukijumlisha na kodi hadi yamfikie mlaji lazima yataongezeka," alibainisha.

**MMARI NA MAFUTA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti wa Programu za Kumaliza Umaskini (REPOA), Dk. Donald Mmari, amesema uhaba wa dola duniani kwenye uchumi umesababisha bei ya mafuta kupanda.

Alisema uhaba wa dola duniani kwenye uchumi kwa maana ya kupanda thamani ikilinganishwa na sarafu zingine, kumesababisha mafuta kupanda. Alisema nchi zinazozalisha mafuta zimepunguza uzalishaji na kufanya bei ipande ili kupata mapato zaidi na kusababisha nchi ambazo hazizalishi kuathirika zaidi.

**WAUZAJI MAFUTA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wauzaji wa Mafuta Tanzania (TAOMAC), Raphael Mgaya, alisema kupanda kwa mafuta kunatokana na kuongezeka kwa bei katika soko la dunia.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, thamani ya shilingi imeporomoka kwa kuwa wanaingiza mafuta kwa dola na kuuza kwa shilingi na kwamba thamani ya shilingi inaporomoka, hivyo mafuta gharama itakuwa kubwa kadiri mtu anavyobadilisha viwango vya fedha.

Alisema gharama za usafirishaji zimeongezeka kwa sababu imechangiwa na tenda iliyotangazwa ya muda mfupi na kusababishia tatizo hilo.

Pia alisema bado hali ni tete katika upatikanaji wa dola ambazo zinawawezesha kulipia mafuta kwa kuwa tangu Benki Kuu ya Tanzania (BoT) iweke kikomo kwenye viwango vya kubadilisha dola, upatikanaji wake umekuwa mgumu zaidi.

Juzi, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilitangaza bei elekezi ambayo imepanda kutoka Sh. 3,199 hadi 3,213 ikiwa ongezeko la Sh. 14 kwa petroli huku dizeli ikipanda kutoka 2, 935 hadi 3,259 sawa na ongezeko la Sh. 324.

MKUTANO MIFUMO YA CHAKULA

# Marais 7 kushiriki majadiliano, waziri aonesha fursa tele mifugo

**Na Waandishi Wetu**

MARAIS saba toka Afrika wamethibitisha kushiriki majadiliano na kuja na makubaliano ya kuimarisha mifumo ya chakula barani katika mkutano maalum leo.

Kabla ya mkutano huo, Rais Samia Suluhu Hassan, atawahutubia vijana wa Afrika wanaojihusisha na kilimo na wale walioko katika mnyororo wa thamani wa bidhaa za kilimo.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa wakuu hao wa nchi watashiriki majadiliano ya Kongamano la Mifumo ya Chakula (AGRF), linaloendelea jijini. Kongamano hilo lilianza juzi na litahitimishwa kesho.

"Marais waliothibitisha kushiriki ni saba, wengine wataendelea kuthibitisha kwa sababu mkutano ni kesho (leo), inawezekana wakaongezeka au wakaja kwa uwakilishi. Kila rais atatoa hotuba yake, watapokea taarifa mbalimbali na kutoa maazimio ya mkutano," alisema Msigwa.

"Kesho jioni Rais Samia amealika wageni Ikulu ambapo tuzo ya Mzalishaji Bora wa Chakula Afrika itatolewa," alisema.

Msigwa alisema mkutano huo umewakutanisha wadau wa kitaifa na kimataifa, kutoka ndani na nje ya Bara la Afrika.

"Kwa upande wa Tanzania, serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika sekta hii na sasa bajeti inakaribia Sh. trilioni moja, ili kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo kwa lengo la kuwatoa wakulima katika kilimo cha mazoea cha kutegema mvua," alisema Msigwa.

Kwa miaka mitatu mfululizo, bajeti ya Wizara ya Kilimo imeongezeka. Imepanda kutoka Sh. bilioni 751.12 mwaka 2022/23 hadi kufikia Sh. bilioni 970.78 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 29.24.

**FURSA MIFUGO**

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alisema jana kuwa sekta ya mifugo ina fursa mbalimbali zinazofaa kwa uwekezaji kwa kuwa inagusa maisha ya kaya milioni 2.2 nchini.

Alisema kuna mifugo takribani milioni 77 na ugufaji ni shughuli kubwa ya kiuchumi inayoweza kubadilisha maisha na kuchangia uchumi wa mtu mmoja na taifa kwa ujumla.

Akiwasilisha mada kuhusu hali ya mifugo nchini kwenye mkutano huo, Waziri Ulega alisema ni muhimu kuweka jicho katika sekta hiyo kutokana na mchango wake mkubwa.

Ulega alisema ufugaji unachangia uzalishaji wa kila mwaka wa tani 805,000 za nyama, lita bilioni 3.6 za maziwa, mayai bilioni 5.5, vipande milioni 14.1 vya ngozi na ngozi.

Alisema fursa nyingine ni kuwapo kanda za ikolojia ya kilimo zinazosaidia uzalishaji wa aina tofauti za mifugo, ikiwamo ya Nyanda za Juu Kusini ambako hupendelea uzalishaji wa maziwa, Kanda ya Kati na Ziwa zinazofanya ufugaji wa ng'ombe na mbuzi wa nyama na Kaskazini inayojihusisha na ng'ombe na kondoo.

Alibainisha fursa zingine kuwa ni kuwapo mazingira mazuri na tulivu ya kisiasa nchini, na uwezo wa idadi kubwa ya rasilimali watu wakiwamo vijana na wanawake.

Vilevile, mazao ya mifugo yanachangia ulaji wa kila mtu wa kilo 15 za nyama, lita 62 na mayai 106 kwa mwaka dhidi ya viwango vilivyopendekezwa vya kilo 50, lita 200 na mayai 300.

"Thamani ya mauzo ya nje kwa upande wa sekta ya mifugo ni tani 14,700 za nyama, kilogramu 65,000 za maziwa na vipande 800,000 vya ngozi na ngozi, kwa pamoja zikiingiza zaidi ya Sh. bilioni 61 na dola milioni 2.4," alibainisha Ulega.

KILIMO HAI

Katika hatua nyingine, serikali imeombwa kuwaunga mkono vijana wanaojihusisha na kilimo hai kisichotumia kemikali ambacho kinatunza mazingira na afya za walaji.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Kilimo Hai (TOAM), Dk. Mwatima Juma, aliwasilisha hoja hiyo jana katika kongamano hilo, akisema wakulima wakiwezesha wanaweza kuongeza uzalishaji kwa kutumia samadi na mbolea hai inayotokana na mwani, hivyo kuzalisha ajira na biashara kupitia kilimo hicho.

Mkulima wa Mboga na Matunda, Mwanahamisi Hassan, alisema kilimo hai cha mazao hayo hakina gharama kubwa na kina soko kubwa.

**OFISI YA ATO**

Katika hatua nyingine, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Mpango wa Mabadiliko ya Kilimo (AATI) wamezindua Ofisi ya Mabadiliko ya Kilimo Tanzania (ATO).

Uzinduzi huo ulifanyika juzi jijini wakati wa mkutano wa pembeni mwa kongamano hilo. Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema ofisi ya ATO itasaidia mabadiliko ya kilimo cha Tanzania na kuwa na sekta jumuishi, endelevu na inayoendeshwa kwa ujuzi.

Alisema ATO itakuza mageuzi na ukuaji wa sekta ya kilimo nchini kupitia dira ya utekelezaji wa mikakati, kuongeza uwezo wa serikali katika kutekeleza Mpango Kabambe wa Mabadiliko ya Kilimo na kusaidia utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Mabadiliko ya Kilimo kwa ufanisi na utekelezwaji wa kina.

Waziri Bashe pia alisema ofisi hiyo itasaidia katika kujenga uwezo na kupeleka zana za ufuatiliaji na tathmini katika maeneo husika.

Mkurugenzi Mtendaji wa AATI, Safia Boly alisema wataangalia sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kwa kufuata kanuni na taratibu zilizotengenezwa kwa ajili ya kuendeleza juhudi za serikali.

Waziri wa Ufugaji na Uvuvi, Ulega, alisema kazi kubwa ya ofisi hiyo itakuwa kuangalia kanuni iliyotengenezwa na wizara kama inafuatwa au haifuatwi.

***Imeandaliwa na Restuta James, Maulid Mmbaga, Jenifer Gilla na Renatha Msungu**

## HABARI KITAIFA



Ofisa Mhifadhi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania, Kanda ya Kusini Mashariki, Linus Chuwa (katikati), akitoa elimu kwa wananchi kuhusu namna ya kukabiliana na tembo ili wasiendelee kuleta madhara kwa jamii katika Kijiji cha Mkoka, wilayani Nachingwea mkoani Lindi hivi karibuni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mahakama yaombwa mshtakiwa mauaji ya mkewe na kumchoma mkaa apimwe akili

**Na Kulwa Mzee**

HAMISI Luogo anayeshtakiwa kwa kumuua mkewe Naomi Marijani, kisha kumchoma moto na mabaki ya mwili, majivu kuyafukia katika shimo na kupanda migomba, amekana kufanya mauaji hayo mbele ya mahakama.

Wakili wa mshtakiwa huyo, Mohammed Majaliwa, amedai mahakamani kwamba wanatarajia kuomba amri ili mteja wake akapimwe akili kujua wakati wa tukio hali ya akili ilikuwaje.

Luoga alikana kosa la mauaji ya kukusudia katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam iliyoketi Kituo Jumuishi cha Kutolea Haki Kinondoni, mbele ya Jaji Musa Pomo, baada ya kusomewa maelezo ya awali ya mashtaka yanayomkabili.

Katika shauri hilo upande wa Jamhuri unawakilishwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Doroth Masawe na upande wa utetezi unawakilishwa na Majaliwa, akisaidiana na Wakili Zadad Mikidadi.

Wakili Doroth aliomba kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali na kudai Mei 15, mwaka 2019 eneo la Gezaulole, Kigamboni mshtakiwa kwa makusudi alimuua mkewe Naomi.

Mshtakiwa alipotakiwa kujibu kweli au si kweli, alikana kuua kwa makusudi, lakini Jaji Pomo alitaka jibu moja kati ya kweli au si kweli ndipo mshtakiwa alirudia kujibu si kweli.

Wakili Doroth alidai mshtakiwa Hamisi, ambaye ni mfanyabiashara, wakati wa tukio alikuwa na umri wa miaka 38 na katika ndoa yao walifanikiwa kupata mtoto mmoja.

Ilidaiwa Mei 19, 2019 mshtakiwa aliripoti Kituo cha Polisi Mji Mwema kwamba mkewe katoweka na mtoto tangu Mei 15, 2019.

Mshtakiwa alipohojiwa polisi alikiri kuua, alichukua mwili wa marehemu na kuupeleka kwenye kibanda akauchoma moto kwa mkaa.

Ilidaiwa mshtakiwa alichukua mabaki ya mwili na majivu na kuyapakia katika gari na kwenda kuyazika katika mashimo aliyoandaa maeneo ya Mkuranga na baada ya kufukia alipanda migomba.

Wakili Doroth alidai mshtakiwa aliwaongoza polisi hadi eneo la tukio na kuchukua vinasaba 17, baada ya vipimo vilionekana vina uhusiano na ndugu wa marehemu.

Upande wa mashtaka ulimaliza kusoma maelezo ya awali na mshtakiwa alipopewa nafasi ya kujibu, alidai amesikiliza, lakini kuna vitu vingine vimekaa zigizaga.

Jaji Pomo wakati akimwongoza kujibu kwamba anakubali kipi na anakataa kipi, mshtakiwa alikubali majina yake, umri na mahali alipokuwa akiishi, lakini alikana maelezo mengine yote.

Wakili Doroth alidai upande wa Jamhuri unatarajia kuita mashahidi 28, vielelezo halisi nane ikiwamo simu na laini zake na mabaki ya mwili wa marehemu.

Alidai vielelezo vingine ni nyaraka saba ikiwamo ramani ya eneo la tukio na maelezo ya onyo.

Wakili Majaliwa aliomba mahakama isitaje idadi ya mashahidi wa upande wa utetezi mpaka wakati utakapofika.

Wakili Majaliwa alidai wanatarajia kuiomba mahakama itoe amri mteja wao apelekwe kupimwa akili ili kujua wakati wa tukio akili yake ilikuwaje.

"Mheshimiwa nawasilisha maombi kupitia kifungu namba 219 cha Sheria ya Makosa ya Jinai kifungu kidogo cha (1) (2) sura ya 20 kilichofanyiwa marekebisho mwaka 2022," alidai.

Jaji Pomo aliahirisha shauri hadi Msajili wa Mahakama Kuu atakapopanga tarehe ya kuanza kusikiliza mashahidi.

Pia, alisema maombi ya kumpeleka mshtakiwa kupimwa akili yatasikilizwa tarehe itakayopangwa, kama inafaa aende kupimwa akili au la.

## Jela miaka 3 kwa kummwagia maji ya moto mke mwenza

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MKAZI wa kisiwa cha Kome, wilayani Sengerema, Vumilia Kasomelo (32), amehukumiwa kwenda jela miaka mitatu kwa kosa la kummwagia maji ya moto mke mwenza.

Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya ya Sengerema, Evod Kisoka, alimtia hatiani mshtakiwa baada ya kukiri kosa lake.

Akisoma mashtaka dhidi ya mshtakiwa, Mwendesha mashtaka Morice Mtoi, alidai tukio hilo lilitokea Agosti 26, mwaka huu majira ya saa tatu usiku.

Ilidaiwa kuwa Vumilia alitenda kosa hilo kwa kummwagia maji ya moto Mariam Paulo (36), kinyume na kifungu namba 225 cha sheria ya kanuni ya adhabu sura ya 16 toleo la mwaka 2022.

Mshtakiwa alikiri kutenda kosa hilo kutokana na hasira baada ya kuoneshwa na watu waliokuwa kwenye msiba wa baba mkwe wao kuwa Mariam ni mke mwenzie kwa mume wao, Ndagabwene Evarist (38).

"Nilipata hasira nilivyooneshwa na watu kuwa huyo ndiye mke mwenzangu, ndio nikachukua uamuzi wa kummwagia maji ya moto," alidai Vumilia.

Aliiomba mahakama impunguzie adhabu, lakini alifungwa kifungo hicho ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama hiyo.

# Lissu: Walimu wasisimamie uchaguzi

**Na Elizabeth Zaya**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema kabla ya Uchaguzi Mkuu na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ujao, kuna haja kufanya kila linalowezekana kubadili katiba ili kuwaondoa walimu kuusimamia.

Amesema mabadiliko wanayoyataka katika mfumo huo wa uchaguzi ni pamoja na kuhakikisha walimu na watumishi wengine wa serikali hawasimamii uchaguzi.

Lissu alitoa kauli hiyo juzi jioni wakati akihutubia mkutano wa hadhara uliofanyika Shirati, mkoani Mara ikiwa ni mwendelezo wa mikutano ya chama hicho iliyopewa jina la Oparesheni +255#KatibaMpya inayofanywa na viongozi wakuu wa chama hicho nchi nzima.

"Pendekezo langu ni kwamba kabla ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka ujao na kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2025, tufanye lolote linalowezekana tubadilishe Katiba na mfumo wa uchaguzi.

"Kama tusipofanya linalowezekana kuhakikisha kwamba walimu na watumishi wengine wa serikali hawasimamii uchaguzi tena kama ilivyo kwa nchi nyingine, na kama ambavyo imependekezwa na wasimamizi wa uchaguzi wa kimataifa ambao wanaangalia uchaguzi wetu, mjue kwamba uchaguzi huo utakuwa kama wa 2020.

"Tusipofanya linalowezekana kubadilisha Katiba na kuwa na Tume huru ya Uchaguzi badala ya hii iliyopo sasa, tujue yatatokea ya 2020. Tusipotengeneza sheria na Katiba inayokataza watu kupita bila kupingwa, mjue enguaengua haitoisha," alisema.

Lissu alisema kudai Katiba Mpya pamoja na kubadilishwa mfumo wa uchaguzi ni jukumu la kila mtu na si la CHADEMA pekee.

"Lazima tulazimishe kufanyike mabadiliko katika eneo hili, na kama tusipolazimisha tumekwisha. Na hilo ni jukumu letu sote. Tutengeneze vuguvugu la kitaifa nchi nzima kuhakikisha hatuendi katika uchaguzi ujao bila Katiba Mpya.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
07.09.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumapili tarehe 10-09-2023 kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero kupitia Mikumi, gari hizo zina namba za usajili: **T 914 DSD / T 272 DUH T 183 DFC / T 269 DUH T 679 DUH / T 837 DJB T 778 EAP / T 630 AJA**

2. Gari hiyo ina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu** - **mita 24.00**
   **Upana** - **mita 5.00**
   **Kimo** - **mita 5.20**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi,** gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

MAZUNGUMZO MAALUM

# Slaa aanika msimamo wake kuhusu dini na siasa

## -Agusia kufutiwa hadhi ya ubalozi, Katiba Mpya

**Na Waandishi Wetu**

KATIBU Mkuu mstaafu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Dk. Willibrod Slaa, amesema dini na siasa haviwezi kutenganishwa.

Dk. Slaa ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) kabla ya kuwa mbunge, amesisitiza upo uhusiano wa karibu kati ya siasa na dini katika kuimarisha maisha ya binadamu.

Katika mazungumzo maalum na waandishi wa habari hizi nyumbani kwake Mbweni, Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, Dk. Slaa amewanyooshea kidole watu wanaotaka kutenganisha dini na siasa, akidai wana lengo la kuficha uovu wao.

Mwanasiasa huyo ambaye wiki iliyopita alivuliwa Hadhi ya Ubalozi na Rais Samia Suluhu Hassan, anasema kila kitu kinachoamuliwa na viongozi wa siasa ni muhimu kuhojiwa na wananchi, wakiwamo viongozi wa dini.

"Ni mjinga tu atazungumza hivyo. Hebu nipe tafsiri - dini ni nini na siasa ni nini? Ukinipa tafsiri ya hivyo halafu utaniambia ninajua unarejea kauli ya Rais mstaafu. Viongozi wetu wa kitaifa wanaapa kwa kitabu gani?

"...watu wanazungumza hayo kwa sababu wanafukia madhambi yao kwa kutoa matamko ambayo hayajafikiriwa.

"Tusitafute sababu ya kukwepa wajibu kwa kisingizio cha eti kuchanganya dini na siasa, kwa sababu maji ni siasa, elimu ni siasa. Wewe umeshawahi kuamua mwenyewe juu ya upatikanaji wa maji yako?

"Hata kupanga bomba la maji lipite wapi na liishie wapi, kunaamuliwa na nani kama siyo viongozi wa siasa? Sasa, leo unasemaje tusichanganye dini na siasa?" Dk. Slaa alihoji.

### TUHUMA POLISI

Kuhusu msimamo wao wa kutotii tena agizo la kuripoti polisi kutokana na tuhuma zinazomkabili na wenzake wawili, Dk. Slaa anasema hajawahi kuripoti tena tangu kuachiwa kwa kile anachoamini hana kosa lolote la kumfanya kuripoti polisi.

Anasema vifaa vyake vya kielektroniki ikiwamo simu ya mkononi, hajakabidhiwa tangu vilipochukuliwa na Jeshi la Polisi. Anataka arejeshewe vifaa vyake.

"Niripoti polisi kwa kosa gani? Nilikamatwa kwa uchochezi, nikaandikiwa hivyo pale Oysterbay. Wakaichana wenyewe kwa sababu wamepokea maelekezo na walisema hivyohivyo kwamba 'tumepokea maelekezo shtaka limebadilika', ikageuka kutoka uchochezi ikaenda kuwa uhaini.

"Mtu yeyote anayejua kusoma sheria, anajua kuwa ugaidi na uhaini ndiyo makosa makubwa katika nchi na haya makosa hayana dhamana. Kwahiyo, nilikamatwa, nikabebwa, nikapelekwa Mbeya. Nimefika Mbeya nikawa mtalii mzuri sana.

"Nilikaa katika chumba kimoja cha mahabusu ambacho kinafanana kidogo na hoteli. Nikaishi vizuri pale. Siku ya nne ninafikiri nikaambiwa 'tunageuza', nikabebwa tena. Ninaona tunageuza kurudi Dar es Salaam. Nimebebwa usiku na kurudi. Nikafika tukaambiwa tuweke dhamana na sisi tukaweka.

"Lakini, kesi ya uhaini haina udhamini. Kwahiyo, mpaka sasa sijui nilikamatwa kwa kosa gani, maana kama nipo nje maana yake kesi hiyo haipo. Hiyo inaonesha tusivyojua kufuata katiba na sheria.

"Mimi nilishasema kama ni kwa sababu ya bandari, niko tayari kwa chochote ili kulinda mali za wajukuu. Mimi nimeshafika mwisho wa maisha," anadai Dk. Slaa.

### ANA NJAA?

Kuhusu madai ya kuipinga serikali kwa maelezo kuwa ana njaa na yuko katika mawindo ya uteuzi ili kupata chochote, Dk. Slaa anasema alishastaafu utumishi wa umma na amefikia umri wa uzee, hivyo hahitaji nafasi yoyote ama kuteuliwa au kuchaguliwa.

"Hao wanaosema Dk. Slaa ana njaa, je, wao wameshiba? Kushiba maana yake nini? Maana kila mtu na tafsiri yake. Kushiba kwangu mimi leo ninatamani niwe na ndege hapa nje.

"Nikitaka kwenda Karatu (Arusha), nipande ndege yangu. Ningependa niwe na shangingi la Sh. milioni mia tatu. Kwahiyo, kwa maana hiyo sijashiba.

"Kama ni kwa zile maana za propaganda, basi mimi nimeshiba. Ninakula, ninalala na nyumba yangu ni hii mnaiona. Je, nina shida hapa? Kwahiyo, mtu asiyejua anaongea nini, anayeweza kusema hivyo ni wale watu wa mavuvuzela kama kwenye mpira wa Simba na Yanga," anafafanua.

### KATIBA MPYA

Dk. Slaa ambaye aliwahi kuwa Balozi wa Tanzania huko Sweden, pia amekosoa utaratibu wa kutoa elimu ya Katiba kwa wananchi kwa miaka mitatu. Anadaiwa wananchi wana uelewa wa kutosha, hivyo wanahitaji Katiba Mpya.

Utoaji elimu, kwa mtazamo wake, ni kutaka kutumia mwanya huo kama mbinu ya kuchelewesha mchakato wa nchi kupata Katiba Mpya.

Dk. Slaa anasema wakati nchi inapata uhuru, asilimia kubwa ya wananchi hawakuelewa katiba. Sasa wanao uelewa.

"Leo ukitazama watu wengi zaidi wana uelewa wa Katiba ni nini, serikali inaongozwaje tofauti na wakati wa uhuru. Kama wakati wa uhuru tulipewa uhuru tukiwa hatujui huo uhuru wenyewe maana yake ni nini, alikuwa anajua Mwalimu (Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere) na lile kundi lake la watu wachache, lakini wazungu wakakubali wakatupa uhuru," anasema.

"Na mimi nilishuhudia bendera ya Mwingereza ikishushwa. Mimi sikuhadithiwa kama ninyi. Mimi nilishiriki, nilikuwa kiongozi wa bendi wakati ule. Kwahiyo, nilijua maana yake nini. Leo ninaposikia hivyo kwa waziri, ninafika mahali ninaona Taifa letu limetumbukia," anadai.

Hoja hiyo ya Dk. Slaa inatokana na kauli ya aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, kwamba wananchi wanahitaji kueleweshwa kuhusu Katiba ya mwaka 1977.

Dk. Ndumbaro ambaye sasa ni Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, alisema wiki iliyopita kuwa utafiti umeonyesha zaidi ya asilimia 50 ya wananchi hawana uelewa kuhusu katiba hiyo, hivyo wanahitaji kutoa elimu kwa wananchi kwa miaka mitatu hadi 2026 ndipo mchakato wa kupata Katiba Mpya uanze.

Waziri huyo alidai kuwa bila kufanya hivyo, wananchi watashindwa kutoa mchango chanya katika mchakato wa kupata Katiba Mpya, hoja ambayo imepingwa vikali na wadau mbalimbali wanaojumuisha wanaharakati na asasi za kiraia.

Kama ilivyo kwa Dk. Slaa, wadau hao wanahoja kwamba elimu hiyo ilikwishatolewa na aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Jaji mstaafu Joseph Warioba, tangu mwaka 2011 mchakato ulipoanza.

### HADHI UBALOZI

Kuhusu kufutiwa Hadhi ya Ubalozi, Dk. Slaa anadai hajawahi kuharibu kazi katika kipindi chake cha uwakilishi na hakuwahi kupewa onyo lolote na mamlaka. Badala yake alipewa barua ya pongezi kwa uwakilishi mzuri.

Anasisitiza kuwa utendaji wake kama balozi utabaki historia na kukumbukwa kwa yale aliyoyafanya alipokuwa kazini.

"Ubalozi ni historia, hauwezi kuondolewa kwa barua. Nimekaa miaka minne kama balozi, sijawahi kupata onyo lolote na niende mbele zaidi wakati ninamaliza Oktoba 21, 2021, nilipata barua ya pongezi kutoka Wizara ya Mambo ya Nje, ndiyo msimamizi wa mabalozi wote," anasema.

"Ukiangalia ukutani hizo picha ni nchi nilizokuwa ninawakilisha. Ukiangalia hapo huyo ni Mfalme, ananitambua mimi. Je, ninahitaji yeye anitambue kama balozi?

"Nchi nilizowakilisha kulikuwa na Rais, kulikuwa na Malkia na Wafalme, na wote wanenitambua. Hiyo ni historia. Nitatambuliwa na wanaofahamu kazi zangu," anasema.

Dk. Slaa aliteuliwa kuwa Balozi na Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli mwaka 2017. Ameiwakilisha Tanzania katika nchi za Nordic (Denmark, Norway, Sweden, Finland, na Iceland) na Baltic (Estonia, Latvia na Lithuania) pamoja na Ukraine. Alistaafu mwaka 2021.

Alifutiwa Hadhi ya Ubalozi siku ya kwanza ya mwezi huu na Rais Samia kwa sababu ambazo hazikuwekwa wazi.

***Imeandaliwa na Enock Charles, Emmaloveness Mkunda na Mwanahamisi Mussa (TUDARCo)**



Dk. Willibrod Slaa.

HABARI KITAIFA




Balozi wa Canada nchini, Kyle Nunas akisalimiana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna katika mkutano wa kimataifa wa mifumo ya chakula Afrika, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkuu wilaya aagiza kukamatwa wazazi waliomtelekeza mtoto mwenye ulemavu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Wilaya ya Kibiti, Kanali Joseph Kolombo, ameagiza wazazi wa Teresia Noel, watafutwe na kukamatwa kwa kumtelekeza mtoto wao kutokana na hali yake ya ulemavu na kushindwa kutekeleza haki yake ya malezi na elimu.

Kanali Kolombo ameahidi kuwasiliana na Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Mobare Matinyi, anapoishi binti huyo ili wazazi wake wakamatwe kwa kushindwa kufanya majukumu yao na badala yake kumuachia bibi ambaye anamlea na amehitimu elimu ya kidato cha sita na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa mujibu wa sheria.

Aliyasema hayo alipokuwa akifunga mafunzo ya JKT kwa vijana walioshiriki katika kikosi cha 832 KJ, akiwamo Teresia na wahitimu wengine wenye mahitaji maalumu.

Katika hafla hiyo ilibainika kwamba Teresia alitelekezwa na mama yake akiwa na umri wa miezi sita baada ya kugundulika kuwa ana ulemavu wa kutembea na baadaye baba yake aliondoka na wote walimuachia bibi kumlea binti huyo hadi sasa.

Vilevile, Mkuu huyo wa wilaya alisisitiza vijana waliohitimu mafunzo hayo kuzingatia uadilifu na kujiepusha na vitendo vya uhalifu baada ya kurejea kwenye makazi yao.

Aliwakumbusha kuachana na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii na vitendo vya rushwa.

Mwakilishi wa Mkuu wa Majeshi, Brigedia Jenerali Godfrey Nyoni, alisisitiza vijana hao kuheshimu na kuzingatia waliyofundishwa na kwa kufanya hivyo watakuwa wamelitendea haki taifa kutokana na fedha nyingi zinazotumika katika mafunzo hayo.

Kamanda wa Kikosi cha Ruvu JKT, Kanali Peter Mnyani, alisema mafunzo hayo yalianza Juni 19, yamedumu kwa miezi mitatu na kati ya vijana waliokuwapo makundi maalumu walishiriki.

Kutokana na maisha anayoishi Teresia kutoka kundi maalumu, Kanali Mnyani alisema kikosi cha Ruvu JKT kitatoa Shilingi milioni moja kwa binti huyo ili iweze kumsaidia atakapoanza masomo ya chuo kikuu.

Akizungumza kwa niaba ya wazazi wa wahitimu, Dk. Daniel Mushi, ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, alisema wazazi wanatakiwa kuwaruhusu watoto wanaochaguliwa kujiunga na mafunzo hayo kwa kuwa wanayofundishwa yanawasaidia kujiandaa kuondokana na utegemezi.

Pia, ilifanyika harambee ya kumchangia Teresia na zaidi ya Shilingi milioni tatu zilipatikana huku waliokuwa wahitimu mafunzo ya kijeshi Operesheni Kambarage wakiahidi kutoa Shilingi milioni moja na kuendelea kumsaidia binti huyo.

# Jaji Mkuu ahimiza matumizi ya DNA mashauri ya unyanyasaji wa watoto

**Na Mwandishi Wetu**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, amehimiza wadau wanaohusika na utoaji haki, kuongeza matumizi ya vinasaba (DNA) katika ukusanyaji wa ushahidi ili kuwatia hatiani au kuwaachia huru watu wanaotuhumiwa kutenda uhalifu dhidi ya watoto.

Prof. Juma alitoa rai hiyo juzi alipozindua kitabu cha mkusanyiko wa uamuzi wa mashauri ya unyanyasaji wa kingono dhidi ya mtoto wa Tanzania na Ireland, uliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Uzinduzi huo uliratibiwa na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) kwa kushirikiana na Irish Rule of Law International (IRLI).

Prof. Juma alisema kuna matumizi ya DNA nchini katika makosa ya unyanyasaji wa kingono kwa watoto na kutoa wito kuiga nchi ya Ireland ambayo inatumia DNA katika ukusanyaji wa ushahidi na kuamua mashauri hayo.

"Tunashangaa kwanini, huku sheria iko wazi kabisa kwa sababu DNA inaweza kuwatia hatiani na pia kuwaondolea hatia wasio na hatia.

"Je, siyo wakati na sisi pia kupata uzoefu kutoka Ireland jinsi ushahidi wa DNA unavyotumika? Kuna mengi ambayo tunaweza kujifunza kutokana na kitabu hiki kinachoonesha wenzetu wanavyoamua mashauri ya watoto," alisema.

Jaji Mkuu alisema Tanzania inapaswa pia kujifunza mbinu bora ya kurekodi ushahidi wa mtoto kutoka Ireland, ambayo ina vifungu vya sheria vinavyoruhusu ukusanyaji wa ushahidi kwa njia hizo.

Alisema kuwa kitabu hicho kimekuja wakati mwafaka kukiwa na utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Rais ya Mfumo wa Haki Jinai. Baadhi ya mapendekezo yanafanana na yaliyomo katika kitabu hicho.

Naibu Balozi wa Ireland nchini, Margaret Gaynor, aliipongeza Serikali ya Tanzania kwa hatua inazozichukua kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia na namna inavyoendelea kuwajenga uwezo wadau wa masuala ya haki jinai.

Jaji wa Mahakama ya Rufani ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi la IJA, Dk. Gerald Ndika, alisema kitabu hicho kitakuwa nyenzo muhimu siyo tu kwa maofisa wa mahakama, bali pia kwa mawakili, waendesha mashtaka, wapelelezi, watunga sera, wasomi na umma kwa ujumla.

Awali akitoa salamu za ukaribisho, Mkuu wa IJA ambaye pia ni Jaji wa Mahakama ya Rufani, Dk. Paul Kihwelo, alisema watatoa mafunzo kwa majaji na mahakimu kuhusu kitabu hicho ili kufundisha watu wengine kwa lengo la kuhakikisha kitabu kinaleta tija.

"Baada ya kutengeneza kitabu hiki, tutakwenda kwa hatua ya pili kwa kutoa mafunzo kwa wakufunzi ambao ni majaji 15 na mahakimu, watu hao watakwenda kwenye kanda saba nchini ili kutoa mafunzo kwa maafisa wengine wa mahakama," alisema Dk. Kihwelo



## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Pongezi SMZ kuwatambua raia wasiohamishika

**JUZI** Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amekabidhi vyeti vya uraia kwa kundi la wahamiaji wasiohamishika 3,319.

Hatua hiyo inatokana na mataifa mbalimbali duniani hivi sasa kuendelea kuimarisha sheria zao za uhamiaji na uraia kwa lengo la kudhibiti uingiaji, ukaaji na utokaji wa watu ili kulinda mipaka na kuhakikisha amani na usalama katika mataifa yao.

Katika hafla ya kukabidhi vyeti vya uraia kwa wahamiaji hao Dk. Mwinyi amesisitiza Idara ya Uhamiaji yenye dhamana ya masuala ya uhamiaji nchini, kuendelea kuziimarisha sheria zilizopo hususan Sheria ya Uraia wa Tanzania.

Sheria kwa mujibu wa Rais Mwinyi haijafanyiwa mapitio kwa kipindi kirefu na kukumbusha kuwa ni wakati mwafaka wa kuiangalia upya kwa madhumuni ya kuiwezesha kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazowahusu wananchi na wageni wanaofika visiwani humo.

Tukio hilo lililofanywa na Dk. Mwinyi linaandika historia mpya ya kulikamilisha jambo hilo kubwa la kuwapa uraia ndugu zao ambao walioishi nao kwa zaidi ya miaka 50 wakiwa na asili ya mataifa jirani ya Burundi, Comoro, Msumbiji na Rwanda.

Raia hao wakigeni walioishi Zanzibar kwa miongo mitano wamepongezwa kwa kupata hadhi hiyo ya kutambuliwa kuwa raia wa Tanzania baada ya kukamilisha matakwa kwa mujibu wa Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Serikali zote mbili za SM na SMT zimefurahisha kuona hatimaye suala hilo limekamilika kama zilivyotoa ahadi ya kulishughulikia baada ya kuingia madarakani mwaka 2020.

Ndoto ya muda mrefu waliyokuwa nayo ndugu hao sasa imetimia na kukamilika kwa utambuzi huo kunawafanya watambulike kuwa Raia wa Tanzania badala ya wahamiaji wasiohamishika.

Waliokabidhiwa hati hizo sasa watapata heshima inayostahili hadhi ya kuwa raia wema.

Sasa raia hao wana wajibu wa kuendeleza utiifu wa sheria na kujiepusha na vitendo viovu ili wasipotoshe dhamira njema ya serikali ya kuwapa uraia wa Tanzania.

Wanatakiwa kushirikiana kulinda na kudumisha amani iliyopo kwa faida ya sasa na watakaokuja baadaye.

Serikali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Mapinduzi ya Zanzibar zimewasamehe Watanzania hao Shilingi milioni mbili kama kima cha kulipia uraia wao.


Jeshi la Uhamiaji sasa linajukumu la kuratibu masuala yote ya uhamiaji nchini yanayohusu raia wanaoomba uraia kisha kukabidhi kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Idara ya Uhamiaji Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifanya utambuzi kwa Watanzania hao baada ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Watanzania hao waliokuwa wakikosa haki zao za msingi kisheria zikiwamo hati za uraia, hati za kusafiria na haki nyingine wanazopatiwa Watanzania halisi.

Jumla ya Watanzania 3,319 wenye asili ya mataifa mbalimbali waliokuwa wahamiaji wasiohamishika wametambuliwa rasmi. Miongoni mwao 3,116 wanaasili ya Msumbiji, 147 wanaasili ya visiwa vya Komoro, watano kutoka Burundi na raia mmoja kutoka Jamhuri ya Rwanda, watoto 1,675 pia wametambuliwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# TANROADS na TARURA Mwanza rekebisheni taa barabarani, msiibebeshe lawama polisi

Na Anthony Gervas, Mwanza

**MIUNDOMBINU** ya taa za kuongoza magari na watembea kwa miguu, mara zote ni muhimu kufanyiwa matengenezo ya haraka pale inapoharibika, badala ya serikali kusubiri mpaka ajali zisizokuwa za lazima zitokee, ndipo wachukue hatua.

Ni hatua zinachukuliwa, huku maskini wa watu Polisi mkoa na Kamanda mgeni katika mkoa, Wilbroad Mutafungwa, anaangushiwa mzigo wa lawama.

Viongozi na watendaji wanaohusika, nasema kuna haja ya kubadilika kiutendaji, hasa kwa tabia kwa sababu inaonekana imezoeleka miundombinu inapoharibika kutengenezwa au kurekebishwa hadi wapate taarifa za ujio wa kiongozi mkuu kitaifa, Rais, Makamu au Waziri Mkuu, ndiyo watengeneze kwa muda, lakini akiondoka mambo yanarudi vilevile ilivyokuwa zamani.

Barabarani, huduma ya maji bomba kama hakuna ugeni wa viongozi, shida ya maji ni kubwa kwa wananchi, ila anapokuja kiongozi wa ngazi ya juu kwenye ziara ya mkoa, maji yanatoka saa zote kwa kila siku, ila akiondoka tu, hali inarejea ileile maji yanaondoka naye.

Vilevile, barabara hutengenezwa kwa muda wakati siku zote ilikuwa mbovu, watendaji wakidai hakuna bajeti za ujenzi au matengenezo,

Swali la kujiuliza, anapokuja kiongozi wa juu ndio kunakuwapo fedha za dharura za kutengeza na kama hivyo, nidadisi mimi mwana-Mwanza, zinapatikana wapi? Je huo ni uungwana wananchi Watanzania na wana - Mwanza?

Hiyo ndiyo inayosonga hadi kwenye umeme. Kiongozi wa kitaifa akija, taa zinawaka kila siku, hadi amalize ziara yake kikazi, akiondoka, anakwenda nao.

Majibu ya madai ya malalamiko yetu, ni kwamba kuna mgawo wa umeme, kero hiyo inayovuruga shughuli za uzalishaji mali wananchi maskini huwarudisha nyuma kimaendeleo na kiuchumi, tabia hiyo watendaji itaisha lini?

Hapa jijini Mwanza, yapo maeneo na mitaa kuna kero ya taa za kuongezea magari na watembea kwa miguu zimeharibika, lakini wahusika wanajifanya hawajui na kuliachia jeshi la polisi kitengo cha usalama barabarani mzigo huo, hasa inapotokea ajali ndiyo wanaotupiwa lawama na wananchi kuwa ni wazembe.

Kumbe ni kazi ya Wakala wa Barabara Tanzania Mkoa wa Mwanza (TANROADS), pamoja na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini(TARURA), lakini kwanini mnakwepa majukumu yenu kutimiza?

Mjini Mwanza, katika Barabara ya Nyerere Road karibu na mnara, pamoja na stendi za daladala za abiria, taa za kuongoza wavuka kwa miguu ni mbovu hazifanyi kazi, pia Mtaa wa Ghana, Barabara ya Uwanja wa Ndege, hakuna taa za kuruhusu magari upande wa kulia na kushoto, jukumu lililoko chini ya utekelelezaji wa Tanroads mkoa.

Vilevile, Mtaa wa Uzinza mjini Mwanza, nako katika kituo cha Afya Makongoro na Dampo mjini taa za wavuka kwa miguu, haziwaki kuruhusu kuvuka kwa miguu muda mrefu,lakini hakuna hatua zinazochukuliwa na wahusika wa serikali ambao ni Tarura.

Hali kadhalika Mitaa ya Nyanza na Kaluta, taa za kuongoza magari nako tatizo ni lile lile la kutowaka kuruhusu magari kupita, kwasababu magari yanapita bila kujali hatari kubwa iliyopo kwa wananchi, jambo linaloweza kusababisha ajali mbaya muda wowote.

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania,Mkoa wa Mwanza,(TANROADS) Mhandisi Ambrose Pascal namsikia akisema kuwa taa za kuongoza magari na watembea kwa miguu zinazowahusu wao zitatengenezwa katika mwaka huu wa fedha ulioanza 2023, hivyo tusubiri fedha za serikali na zile za mitaa zinawahusu Tarura.

Mhandisi Pascal anaiomba Mamlaka ya udhibiti Usafiri Nchi Kavu (LATRA), kuyapiga marufuku mabasi ya abiria ya mikoani kuweka kituo cha kushusha abiria eneo la Nata katika kituo cha daladala, ambayo yanasababisha kero na msongamano wa watu kwenye eneo hilo.

Nami nauliza, kwanini Tanroads na Tarura hamtaki kushirikiana na jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama barabarani, ili kuondoa kasoro hizo, badala yake inapotokea ajali mbaya lawama zote za wananchi huangukia Polisi Usalama Barabarani, bila ya kujua kwamba wahusika wa moja kwa moja mko pembeni?

# Askari zaidi 700 waliopigana vita kuu ya pili ya dunia kulipwa fidia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa kamati maalum iliyoundwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imependekeza kuuza mali zisizo na utata za zaidi ya Sh. bilioni 15.9 ili kutoa fidia kwa askari 737 waliopigana vita kuu ya pili ya Dunia.

Fidia hiyo itatolewa kwa askari walio hai 57 na kwa warithi wa askari 680 waliokwishafariki.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kibaha Mjini (CCM), Sylvester Koka.

Koka alihoji kuna mkakati gani kuhakikisha wazee waliopigana vita ya pili ya Dunia chini ya Chama cha TLC wananufaika na mali zao.

Waziri Tax alisema kutokana na maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan, Julai, 2022 wizara iliunda kamati hiyo kwa ajili ya kuchambua na kutoa ushauri kuhusu hatima ya askari hao waliopigana mwaka 1939 -1945 na kuhusu mali za chama cha Tanzania Legion & Clubs (TLC).

"Tathmini iliyofanywa na kamati, ilibaini kuwa askari waliopigana vita kuu ya Dunia walikuwa 737, kati yao 57 wapo hai na 680 wamekwishafariki."

"Tathmini ilionyesha pia kuwa TCL, ina mali zenye thamani ya Sh. bilioni 37.3, hata hivyo, baadhi ya mali hizo zina madeni na zingine zipo chini ya usimamizi au umiliki wa taasisi nyingine na hivyo kusababisha mashaka kuhusu umiliki wake," alisema.

Alisema mali zilizothibitishwa kuwa za TLC bila utata zina thamani ya Sh. bilioni 15.9 na ilionesha pia kuwa, maveterani walio hai wanahitaji matunzo ikiwa ni pamoja na bima ya afya.

"Kamati imetoa mapendekezo ya kuuza mali zisizo na utata za Sh. bilioni 15.9 na kutoa fidia kwa maveterani wote (walio hai, na warithi wa waliokwishafariki), kuwapatia bima ya afya maveterani walio hai na kuwaenzi wote kwa kujenga mnara wa kumbukumbu wa askari wote waliopigana vita hiyo," alisema.

Alisema serikali inafanyia kazi mapendekezo hayo na tathmini kuhusu mali zenye utata inaendelea.

"Huu ndio mkakati wa serikali wa kuwaenzi wazee waliopigana vita ya pili ya Dunia na kuhakikisha wananufaika na mali zao," alisema.



Ofisa Mkuu wa Fedha wa benki ya Exim, Shani Kinswaga (kushoto), akizungumza katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Maofisa Waandamizi wa Jeshi la Polisi, jijini Dar es Salaam juzi, uliongozwa na Mkuu wa Jeshi hilo (IGP), Camilius Wambura. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kanisa Anglikana Mkunazini lapinga Askofu kurudishwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAUMINI wa Kanisa la Anglikana Mkunazini, Zanzibar wamepinga uamuzi wa Askofu Mkuu wa kanisa hilo, Maimbo Mndolwa wa kuitisha kura ya kumrudisha Askofu wa kanisa hilo Michael Hafidh, kinyume na katiba na kanuni ya kanisa hilo.

Wakizungumza na waandishi wa habari kanisani hapo, wazee wa kanisa hilo walisema, Askofu Hafidh anakabiliwa na tuhuma za ukosefu wa maadili, ubadhilifu wa mali za kanisa na matumizi mabaya ya madaraka ambazo hazijatolewa uamuzi licha ya kuundwa tume kuchunguza.

Akisoma tamko hilo, mjumbe wa baraza la wazee wa kanisa hilo, Mwalimu Jane Sudi, alisema miaka mitatu imepita toka tume hiyo imalize uchunguzi na kukabidhi majibu, lakini tangu mchakato wa mashtaka ulipoanza na mpaka sasa wanasubiri majibu.

"Sisi wazee wa kanisa la Anglikana hapa Zanzibar tumeumizwa na kuhuzunishwa sana na mambo yanayoendelea hivi sasa, hayajawahi kutokea kwa askofu mkuu yeyote wa kanisa letu," alisema Mwalimu Jane.

Aidha, aliishauri Halmashauri Kuu ya kanisa ianze haraka utaratibu wa kujisajili kwa mujibu wa sheria za Zanzibar ili kulinusuru kanisa na migogoro inayojitokeza na kutoshughulikiwa.

Alisema kuanzia tarehe ya tamko hilo (juzi) hawatopokea maelekezo yoyote kutoka makao makuu ya kanisa hilo Dodoma wala kwa Askofu Mndolwa, kwa madai kwamba Waanglikana wa Zanzibar wanao uwezo wa kujiongoza wenyewe. "Hapa Zanzibar ndiyo kanisa mama, tunajisimamia wenyewe kama ilivyo kwa Ofisi ya Mufti kwa ndugu zetu Waislamu, hawahitaji Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) kuwasimamia, hivyo hivyo wakristo wa Anglikana Zanzibar hasa kanisa kuu la Kristo Mkunazini, hawahitaji kuongozwa na Askofu Maimbo Mndolwa tena," alisema.

Pia, alisema kikao cha kumrudisha Michael Hafidh kuwa askofu mkuu Zanzibar ni batili na kumsihi asijaribu kulazimisha jambo lolote katika eneo lote la Kanisa Kuu la Mkunazini au Mbweni Zanzibar.

Aliitaka nyumba ya maaskofu kutofumbia macho jambo hilo linalolenga kutaka kuwagawa wakristo wa Zanzibar na kueleza kuwa tukio hilo limewafedhehesha na kuwataka viongozi wa chombo hicho kutenda haki kwa faida ya kanisa na waumini.

Mgogoro unaoendelea katika kanisa hilo chanzo chake waumini wa kanisa hilo kupeleka mashtaka dhidi ya Askofu Hafidh kwenye nyumba ya Askofu Dodoma Septemba 12, 2021 akituhumiwa kwa ukosefu wa maadili, ubadhilifu wa mali za kanisa na matumizi mabaya ya Kanisa ya Ofisi ya Askofu.

Akijibu tuhuma hizo wakati akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Canon Bethel Mlulwa, Katibu kanisa Anglikana Tanzania, alisema siyo kweli Askofu Maimbo hawezi kumrejesha Askofu Hafidh kwa sababu alipewa likizo na nyumba ya maskofu.

"Baraza la kanisa la katiba la Angalikana Tanzania liliketi kutokana na mgogoro huo wa Zanzibar na kufanya maamuzi Askofu Hafidh kwenda likizo, hivyo mtu kwenda likizo ni tofauti na mtu kusimamishwa au kufukuzwa kazi," alisema.

Alisema mwenye mamlaka la kumrejesha Askofu Hafidh katika huduma ni nyumba ya maskofu na siyo Askofu Mndolwa.

Alisema tamko lilotolewa na wazee hao wa kanisa la Anglikana Mkunazini ni upotoshaji usio na sababu yoyote na suala la Askofu Hafidh litarudi katika nyumba ya Maaskofu ambayo ilitoa uamuzi wa kumpa likizo.

Kuhusu madai ya wazee hao kuwa Kanisa la Anglikana Zanzibar linaweza kujitegemea lenyewe, alisema kwa mujibu wa katiba ya kanisa la Anglikana, kanisa hilo kujiendesha haiwezekani.

"Taarifa hii ya kanisa la Anglikana Mkunazini kutaka kujitenga haijafikishwa ofisini kwake na ikiwa wanataka kujitenga upo utaratibu wake ambao ni dayosisi na siyo kanisa moja," alisema. Alisema mgogoro wa Askofu Hafidh haupo kwa dayosisi yote ya Zanzibar bali upo kwa kanisa la Anglikana la Mkunazini pekee na kanisa moja haliwezi kujitenga.

## KABWELA — Na Fadhili Mohammed



# 'Ushuru mkubwa ni kikwazo kwa wakulima'

**Na Restuta James**

MNUNUZI wa mazao katika Wilaya za Malinyi, Mlimba na Ifakara, mkoani Morogoro, Dick Lukala, ametaja ushuru mkubwa wa mazao ni moja ya changamoto zinazoumiza wakulima.

Vilevile, ameshauri ruzuku inayotolewa na serikali kwa wakulima isiishie katika mbolea tu, bali pia itumike kusaidia upatikanaji mbegu na viuatilifu kwa wakulima.

Katika mjadala wa 'Ubunifu na Teknolojia' ulioendeshwa na Msaidizi wa Rais wa Masuala ya Uchumi, Dk. Blandina Kilama, kwenye Kongamano la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) linaloendelea jijini Dar es Salaam, Lukala alisema kumekuwa na tofauti kubwa ya ushuru wa mazao kutoka wilaya moja hadi nyingine, jambo ambalo haliwanufaishi wakulima.

"Hivi juzi tu wilayani Mlimba, ushuru wa mpunga umepanda kutoka Sh. 2,500 kwa gunia hadi Sh. 5,000 na gunia la kilo 100 la mchele limepanda kutoka Sh. 3,000 hadi Sh. 5,000.

"Hakuna mfanyabiashara atakayekubali kubeba gharama hizo. Mwisho wa siku mkulima aliyetakiwa kuuza kilo moja kwa Sh. 2,000 atauza kwa Sh. 1,900. Serikali inapopandisha ushuru inamuumiza mkulima wa chini," alihadharisha.

Lukala alisema ushuru wa pumba laini ambayo ni chakula cha mifugo, nao umepanda kutoka Sh. 300 hadi Sh. 2,000.

Alibainisha kuwa wilayani Malinyi, ushuru wa mahindi umepanda kutoka Sh. 2,500 hadi Sh. 4,000 kwa gunia na kwamba gharama hizo zimepanda bila kuwashirikisha wadau.

"Hivi vitu hatushirikishwi, tunaletewa tu ushuru, lakini anayeathirika hapa ni mkulima ambaye atalazimika kulipa gharama za ushuru kwenye kila kilo ya mazao yake, mwisho wa siku kama ilikuwa auze kilo kwa Sh. 2,000 itabidi auze kwa Sh. 1,900," alisema.

Alisema kampuni yake ya DICLUKALA CO. LTD, imeingia mikataba na wakulima 20,000 katika wilaya hizo ili kuwahakikishia soko la mazao yao na pia kuwasaidia wakopeshe zana za kilimo yakiwamo matrekta.

"Mkutano huu (AGRF), utakuwa na maana kubwa kama serikali zitakuja na mfumo utakaowanufaisha wakulima hasa wadogo," alisema.

Mjasiriamali wa teknolojia za kilimo kutoka Kenya, Esther Kimani, alisema wabunifu wachanga wanakabiliwa na changamoto ya mitaji na mlolongo mrefu wa kusajili biashara kwenye baadhi ya nchi za Afrika.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), John Ulanga, alitoa rai kwa serikali kuweka mifumo itakayowawezesha wenye mitaji kuwekeza kwa kampuni changa na mawazo yenye ubunifu.

"Kama tunavyoangalia watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano, ndivyo tunavyopaswa kulea kampuni changa na mawazo yenye ubunifu.

"Mathalani, serikali inaweza kuja na sera inayotoa unafuu fulani kwa maduka makubwa, yanazouza bidhaa za wajasiriamali wadogo," alisema.



Waziri wa Maendeleo ya Kimataifa wa Norway, Anne Beathe Tvinnereim (wa pili kulia) na Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde (wa tatu kulia), wakipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya mbolea ya Yara Tanzania, Winstone Odhiambo (kushoto), kuhusu uzalishaji wa mbolea walipotembelea kiwanda cha kampuni hiyo, Kurasini jana, ikiwa ni sehemu ya mkutano wa Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) unaoendelea jijini Dar es Salaam. Kulia ni Rais na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Kimataifa ya Yara, Svein Tore Holsether. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watafiti watoa mbinu kuvutia vijana kushiriki katika kilimo

**Na Jenifer Gilla**

WATAFITI wa mazao ya kilimo wameishauri serikali kushirikiana nao kuongeza ushiriki wa vijana katika kilimo kwa kutatua changamoto zinazoathiri ubora wa mazao na soko la kimataifa.

Pia wamesema vijana wengi wanaoshiriki katika kilimo wanakatishwa tamaa na kutokuwa na tija katika uzalishaji kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo afya ya udongo na mbegu.

Waliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam katika mkutano wa pembeni mwaka Kongamano la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) uliojadili namna ya kuboresha afya ya udongo ili kuzalisha mazao yenye rutuba na kujihakikishia usalama wa chakula.

Mtafiti wa Udongo kutoka Taasisi ya Alliance Biodiversity International, David Guerena, alishauri serikali kutumia utafiti wa kilimo unaofanyika nchini kama kigezo cha kuongeza ushiriki wa vijana katika sekta hiyo.

Alisema watafiti wanafanya kazi kubwa kuboresha mnyororo wa thamani ya mazao ya kilimo kama vile mbegu bora na virutubisho vya kuweka katika udongo ili kutoa mazao bora, vitu ambavyo vinakatisha tamaa vijana kushiriki katika kilimo.

Alisema Tanzania ina vijana wengi wanaotoka vijijini kwenye ardhi ya kutosha kulima, lakini wanaishi bila ajira licha ya kuwa na elimu, ujuzi na nguvu za kufanya kazi. "Kwahiyo, tukiweza kufanya kazi pamoja na serikali na mashirika binafsi, tunaweza kusaidia vijana kwenda shambani wakiwa na ujuzi wa kutosha. Kwahiyo, tunahitaji kusaidiana," alisema Guerena.

Alisema kwa muda waliofanya utafiti katika kilimo nchini, wamegundua afya duni ya udongo ni moja ya sababu kubwa zinazopunguza tija kwenye mazao ya kilimo na kusababisha vijana kukimbia kilimo ikiwamo maeneo ya kusini mwa nchi kama vile Iringa, Songwe na Mbeya na Kanda ya Ziwa, hasa Bukoba, mkoani Kagera.

Mkurugenzi wa Ushirikiano wa Kimkakati wa Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya YARA International, Oystein Botillen, alisema katika kukabiliana na changamoto ya udongo dhaifu wa kilimo, wamekuwa wanatoa elimu kwa wataalamu wa kilimo na wakulima hasa vijana kuhusu kuboresha afya ya udongo kwa kutumia unga wenye virutubisho unaojulikana kitaalamu kama lime.

"Kila kitu kwenye kilimo kinaanzia kwenye udongo. Kwahiyo, ukiwa na rutuba ndani ya udongo, mmea utakuwa vizuri," alisema.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, serikali inakaribisha wadau kuwekeza nchini ili kuboresha mnyororo wa uzalishaji chakula.

Alisema pia serikali imejidhatiti kuongeza ushiriki wa wanawake na vijana katika kilimo kwa kuwaandalia mazingira rafiki ikiwamo kuboresha mbegu na udongo ili kuongeza uzalishaji.

# Wakulima wadogo kufadhiliwa

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU moja baada ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, kusisitiza umuhimu wa nchi za Afrika kuwezesha wakulima wadogo, Benki ya NMB imeahidi kuendelea kulifadhili na kuliunga mkono kundi hilo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi.

Dk. Mpango, akizindua Kongamano la Mifumo ya Chakula Afrika ((AGRF) juzi, alihimiza serikali za Afrika kuchukua hatua kuwapa wakulima wadogo pembejeo za bei nafuu, maarifa, ujuzi na fedha ili kuongeza tija katika minyororo ya thamani ya chakula.

Katika mkutano huo jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, mbali na kuonesha utayari huo wa kuliunga mkono kundi hilo, alibainisha jinsi taasisi hiyo inavyoshirikiana na kusaidia wakulima hao kupitia huduma na masuluhisho mbalimbali ya kifedha.

Kiongozi huyo alisisitiza umuhimu wa taasisi za fedha kuchangia kuwawezesha wakulima wadogo kiuchumi.

Zaipuna alisema ujio wa mifumo ya kidijitali umesaidia kuondoa vizingiti vilivyokuwa vikiwakwaza wakulima kukopa kwa urahisi na kupata huduma nyingine za kifedha.

"Taasisi za fedha bado zina kazi ya ziada katika kuwakwamua wakulima wadogo kiuchumi, wengi wao wakiwa wanazalisha kwa ajili ya kujikimu tu huku wakiishi katika umaskini uliokithiri," alisema kiongozi huyo wakati wa mjadala wa Jinsi Sekta Binafsi Inavyoweza Kuwasaidia Wakulima Kuongeza Utoshelevu wa Chakula na Usalama wa Lishe barani Afrika.

Mjadala huo uliandaliwa na OCP Africa kwa kushirikiana na Fertilizer Canada pamoja na Baraza la Biashara Duniani Linalojihusisha na Maendeleo Endelevu (WBCSD).

Mkutano huo wa siku nne, unalenga zaidi kujadili mabadiliko ya mifumo ya chakula na kuhakikisha uhakika wa chakula kwa watu wote barani Afrika.

Akizungumzia mchango wa taasisi kubwa za fedha kama NMB katika kuwawezesha wakulima wadogo wa Afrika kiuchumi, Zaipuna alisema kuwafadhili ni suala la msingi kutokana na umuhimu wao kiuchumi na katika maendeleo ya sekta ya kilimo.

Takwimu zinathibitisha umuhimu huo kwa kuwa wao ni asilimia 90 ya wakulima wote katika nchi zilizoko kusini mwa Jangwa la Sahara na ni wazalishaji wa asilimia 80 ya chakula chote kinachopatikana katika eneo hili.

Kwa mujibu wa Zaipuna, ugumu wa upatikanaji wa huduma za kifedha umekuwa kikwazo kikubwa kwa wakulima wadogo kuweza kufikia uwezo wao wa kiuchumi, changamoto ambayo benki hiyo inapambana kutatua kupitia jitihada mbalimbali.

Juhudi hizo ni pamoja na kubuni suluhisho la kifedha kidijitali, programu maalum za kuwajenga uwezo wakulima pamoja na kampeni za uhamasishaji kama ile ya Teleza Kidijitali ambayo Zaipuna alisema ni promosheni ya mwaka mzima inayoendelea nchini kote kwa sasa.

"Tunaamini kwa dhati kwamba kuwashirikisha na kuwajumuisha kifedha wakulima wadogo ni njia sahihi ya ustawi wao na kuwakwamua kutoka katika lindi la umaskini," aliwaambia washiriki wa mjadala huo.

Alisema hilo linatokana na ukweli kwamba upatikanaji bidhaa na huduma nafuu za kifedha - kama vile akiba, mikopo na bima - ni njia mwafaka ya kusaidia kuboresha maisha ya wakulima hao.

Zaipuna alisema benki hiyo inaendelea kuwekeza kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma zake kwa kutanua mtandao wa matawi yake na kuongeza idadi ya mawakala pamoja na huduma za kidijitali.

Alisema benki hiyo pia imekuwa ikibuni bidhaa mpya na za kisasa pamoja na masuluhisho yanayozingatia na kukidhi mahitaji na matakwa ya wateja wakiwamo wakulima wadogo.

Zaipuna alisema utafiti unaonesha kuwa wengi wao wamekuwa wanakwama kupata ufadhili, jambo ambalo linapelekea wengi kukopa kutoka kwenye vyanzo visivyo rasmi hususani ndugu, jamaa na marafiki.

Katika kutatua changamoto hiyo, alisema benki hiyo imeanzisha huduma ya Mshiko Fasta inayowawezesha wateja kukopa hadi Sh. 500,000 kwa kutumia simu za mkononi.

Kama sehemu ya kutekeleza ajenda ya ujumuishaji kifedha, NMB imekuwa inafungua akaunti mpya za wateja milioni 1.2 kila mwaka, hatua ambayo Zaipuna alisema inasaidia kuwajumuisha wakulima kwenye mifumo rasmi ya huduma za kifedha.



HABARI KANDA KASKAZINI

# Magonjwa yanayohusisha wanyama, binadamu kudhibitiwa

**Na Godfrey Mushi,** HAI

IDARA ya maafa iliyoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, imeanza kuchukua hatua za kukabiliana na madhara yanayosababishwa na mlipuko wa magonjwa yanayohusisha wanyama, mimea na binadamu katika Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro.

Dk. Henry Kissinga, ambaye ni mtaalamu mbobezi wa udhibiti wa maafa hayo, alisema serikali imeamua kupambana na maafa hayo katika mikoa minne, yenye tishio hilo ikiwamo Kilimanjaro.

Kwa sasa, Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Maafa, inaendesha mafunzo ya kujenga uwezo kwa wataalamu wake kutoka sekta za afya ya binadamu, mifugo, mazingira, kilimo na maliasili.

"Lengo letu ni kutengeneza timu itakayojulikana kama 'timu ya afya moja' yenye jukumu la kuratibu vikao na kusimamia shughuli za afya moja, kuandaa mipango mikakati na upatikanaji wa fedha, kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za afya moja.

Zaidi Dk. Kissinga alieleza: "Tunawajengea huo uwezo ili kukabiliana na magonjwa hususani magonjwa yanayotoka kwa wanyama kuja kwa binadamu (Zoonotic). Nia yetu ni ili waweze kutumia dhana ya afya moja itakayozisaidia sekta hizo kukabiliana na magonjwa kwa kuzuia na kuhakikisha kuwa jamii inakua salama, wanyama na mazingira."

Ofisa Maafa wa Wilaya ya Hai, Msafiri Msuya, ameipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kutoa mafunzo hayo, kwa kuwa yanawajengea uelewa wa dhana ya afya moja katika kukabiliana na majanga mbalimbali.

"Elimu hii itatusaidia, kwa sababu tulipokuwa tukifanya kazi, kila mmoja alikuwa anapita katika njia yake. Sasa tunakwenda kufanya kazi kama timu moja, jambo ambalo litasaidia kutotumia rasilimali nyingi katika jambo moja kama ilivyokua hapo awali,"alisisitiza Msuya.

Afya moja ni dhana ya kimataifa, iliyoridhiwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika linaloshughulikia na Afya ya Wanyama (OIE), Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Programu ya Kimataifa ya Mazingira (UNEP), kupitia Mradi wa Global Health Security Agenda (GHSA).

# Vijana 4,500 K'njaro kunufaika kilimo, ugavi, elimu

**Na Godfrey Mushi,** HAI

VIJANA zaidi ya 4,500 wilayani Hai mkoani Kilimanjaro, wako mbioni kubadili hali zao za maisha kiuchumi, baada ya wadau watatu wa maendeleo kuingia makubaliano ya kutekeleza miradi ya kuwawezesha vijana wa kike na kiume kupitia sekta za kilimo, fursa za usafirishaji, ugavi na elimu ya stadi za maisha.

Wadau hao ni Taasisi ya HRNS Tanzania (Hanns R. Neumann Stiftung), Khune Foundation na Shirika la DSW (Deutsche Stiftung Weltbevolkerung).

Kwa mujibu wa Meneja Miradi wa Shirika la DSW Tanzania, Winnie Muine, alisema vijana hao kutoka maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo, watapiga hatua moja mbele katika maendeleo ya kiuchumi kutokana na nguvu kubwa iliyowekwa na wabia hao.

Jana, Muine, alisema mradi huo utakaohusisha wabia hao wa maendeleo,unalenga kuwawezesha vijana kuboresha maisha yao katika maeneo ya afya, elimu, kipato na ustawi wao kwa ujumla ili waweze kufikia malengo yao.

Katika utekelezaji wa mradi huo, kila shirika linalo jukumu lake binafsi, ambapo HRNS Tanzania, wameingia makubaliano na serikali na kujikita zaidi katika masuala ya kuwawezesha vijana wa kike na kiume kwenye sekta ya kilimo, wakati Khune Foundation, wao wataweka nguvu kutoa fursa za elimu ya juu na vyuo vya ufundi, hasa maeneo ya uratibu, usafirishaji na ugavi.

Alisema DSW Tanzania, wao wameingia makubaliano ya kujikita kutoa elimu ya stadi za maisha, kupinga ukatili wa kijinsia, elimu ya afya ya uzazi na utumiaji na upatikanaji wa huduma rafiki kwa vijana.

"Mradi hii kimsingi, inalenga kuwanufaisha kwa kuwawezesha vijana kuboresha maisha yao katika nyanja za afya, elimu, kipato na ustawi wao kwa ujumla ili waweze kufikia malengo yao".

"...Mradi huu wa vijana unaoitwa, Enhancing Livelihood Prospects for Young People, unatekelezwa katika wilaya nne za Mkoa wa Kilimanjaro, ukihusisha Wilaya ya Hai, Rombo, Siha, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi (vijijini)."

Mikoa mingine inayotekeleza mradi huo wa miaka minne kuanzia mwaka 2023 hadi 2027, ni Arusha, Mbeya na Songwe. Katika maeneo hayo, mradi huo utawanufaisha vijana 50,000.

Akizungumzia ujio wa mradi huo, Ofisa Rasilimali Watu, Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro, Amos Machilika, aliwasihi wadau hao kufanya kazi kwa karibu na serikali ili kuhakikisha wanajua vipaumbele vya serikali Kilimanjaro pamoja na fursa zilizopo.




Diwani wa Kata ya Misozwe, wilayani Muheza, mkoani Tanga, Jestina Mntangi, akishiriki kuchimba mtaro katika harambee ya uzinduzi wa ujenzi wa ofisi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya kata hiyo juzi. Wengine ni Mbunge mstaafu wa Muheza, Hebert Mntangi (wa tatu kushoto) na (wa pili kushoto) ni Katibu wa CCM Misozwe, Fakii Masimba. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wakosa maji siku 90, wanunua ndoo moja kwa 1,000/-

**Na Getrude Mpezya,** MONDULI

WANANCHI wa Kitongoji cha Sinoni Kusini kilichoko Kata ya Engutoto, Wilaya ya Monduli mkoani Arusha, wananunua maji ya kunywa na kupikia, ndoo moja kwa Sh. 1,000 kutokana na kukosa huduma ya majisafi na salama kwa muda wa miezi mitatu sasa.

Hali hiyo imekuwa ikisababisha kila uchao wananchi hasa wanawake na watoto wa jamii ya kifugaji ya kimasai, kutembea umbali mrefu kutafuta maji kutokana na eneo hilo kukosa huduma.

Kwa nyakati tofauti, wakizungumza na Nipashe jana katika mahojiano maalum, wananchi hao walisema kwa kuwa makali hayo ya kukosekana maji yanaziumiza familia zao na kuvunja ndoa, wanaiomba serikali kuishinikiza Ofisi ya Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), kutafuta ufumbuzi wa haraka wa adha hiyo.

Kalista Faustine, alisema Kitongoji cha Sinoni Kusini, kiliacha kupata huduma ya maji, tangu Juni, mwaka huu.

"Tunaambiwa tu kwamba sababu ni mtambo wa kusukuma maji kuharibika. Kiukweli tuko gizani hatujui lini tutapata huduma. Tunamwomba Waziri wa Maji, Jumaa Aweso na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela kuja kuzungumza na wananchi".

"Tunaamini serikali ni sikivu na itamwajibisha anayezembea kazini. Waliopewa mamlaka ya kusimamia maji katika wilaya yetu, wako kimya na hawajali kama wananchi wa vijijini tunaumia."

Aidha, Kiria Laitayok, alisema tatizo hilo limewasababishia kuingia gharama ya kununua maji yanayopelekwa kijijini kwa kutumia maboza au madumu, yakiuzwa kwa Sh. 1,000.

"Kutoa shilingi 1,000 ni kitu ambacho kwa mwananchi mwenye familia na kipato cha chini, hawezi kuhimili gharama hiyo. Ndio maana tunamuomba Waziri (Aweso) na Mkuu wa Mkoa (Mongela) waje watumbue wasiotosha katika nafasi zao," alisema Laitayok.

Vilevile, Elizabeth Joshua, alisema hata inapotokea maji yapo, watoa huduma kwa maana ya wafanyakazi wanaogawa maji maeneo mbalimbali, wanafanya upendeleo kwa baadhi ya maeneo.

Thomas Laizer, mjumbe wa Serikali ya Kijiji, alisema wananchi wa Sinoni Kusini, hawana imani na Meneja wa Maji wa RUWASA, Wilaya ya Monduli.


"Tuliahidiwa kwamba tungepata maji Julai 2 mwaka huu lakini mpaka sasa ni Septemba hakuna maji. Kibaya zaidi, wanakuja majumbani wale wasoma mita wao, na wanalazimisha tuchangie shilingi mia tano kila msoma mita atakapofika eneo lako," alieleza Laizer.

Diwani wa Engutoto, Nelson Lowassa, licha ya kukiri kuwapo tatizo hilo, aliiomba serikali kuongeza nguvu katika usambazaji wa maji kwa njia ya maboza ili kukidhi mahitaji ya wananchi wakati mamlaka husika inashughulikia jambo hilo.

Meneja wa RUWASA, Wilaya ya Monduli, aligoma kuzungumzia malalamiko hayo, kwa madai kuwa hadi apewe kibali na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo.

Alipoulizwa kuhusu malalamiko hayo, Mbunge wa Monduli, Frederick Lowassa alisema: "Changamoto kama hizi zinazotokea, zinafanya maisha ya wananchi kuwa magumu. Nimeambiwa pampu za maji, zimeharibika na serikali inafanya juhudi za kuzitengeneza".

"Lakini niwadokeze tayari pampu nyingine zimeshaagizwa na ziko njiani zinakuja kwa ajili ya kutatua tatizo hilo kubwa, na kero ya maji Monduli itakuwa historia."





# WAMACU yajigamba utatuzi kero upatikanaji pembejeo

**Na Timothy Itembe,** MARA

CHAMA Kikuu cha Ushirika cha Wakulima wa Mkoa wa Mara (WAMACU) kimeweka mkakati maalumu wa kuhakikisha kinatatua kero ya ukosefu wa pembejeo kwa wakulima.

Kauli hiyo imetolewa na Meneja Mkuu wa WAMACU, Samweli Gisiboye, wakati wa kikao cha cha bodi kilichofanyika wilayani Tarime.

Kikao hicho kililenga kujadili na kupitisha utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya chama hicho, kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

"Wakulima wa Mkoa wa Mara bado wanakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa pembejeo, lakini tumemejipanga kuhakikisha suala hili linatatuliwa ipasavyo na linakuwa sehemu ya jukumu la WAMACU kwa kila mwaka na kufanya ukosefu pembejeo hizo ni pamoja na mbolea mbegu na viatilifu linakuwa historia" alisema Gisiboye.

Alisema WAMACU kinajipanga kwa baadaye kuanza kuagiza pembejeo kutoka nje kwa kibali cha TFRA na mamlaka nyingine za serikali zinazohusika, badala ya kutegemea wasambazaji wa sasa.

Aidha, alieleza kuwa chama kinaichukulia huduma ya pembejeo kwa wakulima kama fursa na kujipanga kuwa sehemu ya soko la mazao ili kuendeleza na kukuza uzalishaji unaotokana na misukumo inayotolewa na serikali, lengo likiwa ni kulinda na kuhamasisha uzalishaji wenye tija katika Kanda ya Mara.

Mwenyekiti wa chama hicho, David Hechei alisema chama kinaendelea na mkakati wa kuhakikisha kuwa mbolea inaendelea kuwafikia wakulima kwa ukaribu usiozidi kilomita 10 pindi wanapokuwa wameipokea.

Juzi, Ofisa Kilimo na Uvuvi wa Halmashauri ya Tarime Mjini, Fredrick Juma aliliambia baraza la madiwani kuwa upatikanaji wa mbolea kwenye vituo unatakiwa usizidi kilomita nane kutoka kituo hadi kituo.

Meneja Utafiti wa Mipango wa Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI), Alumas Hamadi, kutoka kituo kidogo cha Sirari ambacho kinahudumu katika mikoa ya Mara, Mwanza na Geita alisema WAMACU wanapaswa kuhakikisha wanapata miche bora kwa wakulima.

Alisema, wanashirikiana kwa ukaribu kwa sababu miche yote inayotoka AMCOS ambayo zinatengeneza ushirika ndizo ambazo wanazipatia miche na zina-

## Ujenzi barabara ya changarawe washusha gharama za maisha

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

WANANCHI wa Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wameeleza namna ujenzi wa barabara za changarawe zilivyowaondolea adha ya kupanda kwa gharama za usafiri na bidhaa madukani.

Hayo waliyabainisha jana kwa nyakati tofauti wakati wa ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa Barabara ya Mwabomba, Bugomba 'A', Ulowa, Uyowa yenye urefu wa kilometa 93.

Mkazi wa Kata ya Mwabomba Halmashauri ya Ushetu, Japheti Daudi alisema awali kabla ya ukarabati wa barabara hiyo gharama za maisha zilipanda mara mbili hususani upande wa bidhaa na walipokuwa wakihoji kwa wauzaji walidai gharama za kuleta mzigo ni kubwa.

Alisema wanaishi mpakani mwa Mkoa wa Geita na mahitaji yao wanayapata huko na gharama kutoka Mwabomba hadi Masumbwe ilikuwa ni Sh. 5,000 kwa gari na Sh. 10,000 hadi 15,000 kwa pikipiki.

Alisema kutokana na ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe gharama imeshusha hadi Sh. 2,000 kwa gari na Sh. 4,000 kwa pikipiki.

Mkazi wa Ulowa, Anna Paul alisema ili barabara hizo ziweze kudumu kwa muda mrefu ni vema zikajengwa mitaro na madaraja ya kupitishia maji nyakati za mvua.

"Eneo hili linamachimbo madogo ya dhahabu na wamiliki wake wanapitisha magari makubwa yaliyobeba mawe na mchanga unaosadikiwa kuwa na madini, uzito wake hauendani na barabara hizo, TANROADS isipokuwa makini kuliangalia hili watakuwa wakifanya ukarabati mara kwa mara" alisema Paul.

Meneja wa TANROAD Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Mibara Ndirimbi alisema serikali kupitia Wizara ya Ujenzi kila mwaka imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Sh. bilioni 15 zilitolewa.

Pia alisema kwa mwaka huu wamepokea Sh. bilioni 13.38 kwa ajili ya kukarabati na kufungua barabara mpya katika halmashauri sita, kati ya hizo Sh. bilioni 10.69 ni kutoka mfuko wa barabara na Sh. bilioni 2.69 kutoka serikalini, kwamba barabara zote korofi zinazoharibika kipindi cha mvua zitakarabatiwa.

Alisema tatizo wanalokutana nalo ni ukosefu wa huduma ya maji wakati wa ujenzi wa barabara hali inayosababisha kutumia gharama kubwa za ujenzi na kushindwa kukamilika kwa wakati kulinganisha na maeneo yenye maji ya uhakika.

Alitaja changamoto nyingine kuwa ni uharibu wa miundombinu ya barabara, wizi wa alama za barabarani, uvamizi wa hifadhi za barabara na kujengwa nyumba za biashara ndani ya hifadhi ya barabara.

Meneja matengenezo, mhandisi Midala Yaledi alisema wanatarajia kujenga daraja la kisasa katika Mto Igombe litakalounganisha Mkoa wa Shinyanga na Tabora kwa gharama ya Sh. milioni 586.5.

Alisema hivi sasa wameshapata kibali cha ujenzi, alisema malengo yao ni kufungua mtandao wa barabara maeneo yote.



Meneja Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Mibara Ndirimbi, akiwa kwenye mtambo juzi, akikagua maendeleo ya ujenzi wa barabara mpya inayounganisha Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama na Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora yenye urefu wa kilomita 25 kwa thamani ya Sh. bilioni 3.2. **PICHA: MARCO MADUHU**

## UNESCO yazindua mradi kutokomeza ndoa za utotoni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

TUME ya Taifa ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi na Utamaduni (UNESCO), imezindua mradi wa kupinga ndoa za utotoni wilayani Shinyanga.

Lengo la kuzindua mradi huo ni kuendeleza mkakati wa kupinga ukatili kwa watoto na wanawake wilayani humo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Shinyanga, Tedson Ngwale, alisema mradi huo upo katika muda muafaka wa kupinga ukatili kutokana na wilaya hiyo kuendelea kuwa na matukio ya ukatili kwa watoto.

"Jamii ya Shinyanga bado inakabiliwa na tatizo la ndoa za utotoni, vikiwamo na vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, hivyo kupitia mradi huu wa UNESCO tuna imani matukio haya yatapungua na watoto wetu watasoma na kutimiza ndoto zao," alisema Ngwale.

Naibu Katibu Mtendaji Tume ya Taifa ya UNESCO, Aboud Khamis aliitaka jamii kuwajibika kupinga vitendo hivyo ambavyo vimekuwa na madhara makubwa kwa watoto na kuharibu mfumo wa maisha yao.

Ofisa Programu Mkuu Sayansi ya jamii kutoka Tume ya Taifa ya UNESCO, Uyanjo Lazarus, alisema mradi huo utatekelezwa katika Kata ya Iselamagazi, Ilola na Lyabusalu na kwamba umelenga kuelimisha jamii kuhusu athari za ukatili wa kijinsia na ndoa za utotoni.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Joseph Ntomela, alisema mradi huo utasaidia kupunguza matukio hayo ya ukatili wilayani Shinyanga na watoto wa kike kutimiza ndoto zao.

ama
ALHAMISI SEPTEMBA 7, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



## Ukosefu wa uzio ulivyo mwanya bangi kuvutwa ndani ya bweni

Ukurasa 12



## Kliniki yaweka kambi ya kibingwa bure siku tatu, kurejeshea jamii shukurani

Ukurasa 13

KUTOKA MKUTANO KIMATAIFA WA MIFUMO CHAKULA…

# Utekelezaji mradi BBT aliyopigia makofi Rais '88', wanufaika wake watoa ushuhuda

## •Wadhibiti mazingira, umasikini wakati mmoja...

**Na Jeniffer Gilla**

Ni awamu kadhaa za uongozi wa nchi sasa, wakuu, akiwamo wa awamu ya tano, Rais Jakaya Kikwete, amekuwa akihimiza ufugaji wenye tija, kuwa na mifugo wachache mfugaji anawamudu na inakuwa na tija kwa mazingira.

Katika utawala wa awamu ya sita, chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kaja na maelekezo kuwa na programu mahsusi ya ufugaji na uvuvi wenye tija, kutafutia majibu dhidi ya mifugo mingi, isiyo na tija.

Hapo ndipo wasomi wa mifugo wakakuna vichwa na kuja na majibu ya programu inayoitwa "Jenga Kesho Iliyo Bora" au ( BBT - LIFE), wakiwataka vijana waliopo kwenye programu hiyo kutumia vyema fursa hiyo.

Kweli, utekelezaji wa BBT ukamrudishia Rais Dk. Samia tabasamu katika kilele cha Maonyesho ya Kimataifa ya Wakulima (Nanenane) kwenye viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya, wastani wa mwezi mmoja uliopita.

Katika kauli yake akatamka kufurahishwa namna, wizara inayoongozwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, wanavyosimamia vyema programu ya BBT - LIFE katika sekta za mifugo na uvuvi kwa kuwapatia vijana mafunzo ya vitendo ya unenepeshaji wa ng'ombe, kaa, jongoo bahari, pamoja na kilimo cha mwani.

Amesema soko la nyama nje ya nchi ni kubwa, hivyo kupitia programu ya BBT - LIFE, vijana wanaopatiwa mafunzo ya kunenepesha ng'ombe wanapaswa kutumia fursa hiyo kupata masoko ya kuuza mifugo yao viwandani na hatimaye kuchakatwa nyama za kusafirishwa nje ya nchi.





Mnufaika wa mradi wa BBT, ulioasisiwa na utawala wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, sasa mnufaika akiwa anatoa ushuhuda katika mkutano wa Chakula Afrika, jijini Dar es Salaam. **PICHA: JENIFFER GILLA.**

Rais Dk. Samia, akasema amekuwa akitafuta fedha kwa ajili ya kuhakikisha programu mbalimbali zinaanzishwa na kuendelezwa zikiwamo za ufugaji na samaki, ili vijana waingie katika fursa hizo na kujiongezea kipato, hapo anawataka wazitumie vyema.

Waziri Ulega, naye katika mjumuiko huo wa Naenane, akamueleza Rais Dkt. Samia, namna wizara yao imejikita kuhakikisha programu ya BBT - LIFE inasambaa kitaifa, iwafikie vijana wote.

Anasema lengo la wizara ni kuona sekta za mifugo na uvuvi zinaongeza uzalishaji na kuinua pato la mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Maono ya Rais Dk. Samia, yamekuwa ni kuwapo sekta ya mifugo shindani, inayochangia maendeleo endelevu ya uchumi nchini.

**WAFUGAJI VIJANA WAFUNGUKA**

Katika ukaguzi wa Nipashe ndani ya Mkutano wa Mfumo wa Chakula, unaohitimshwa leo, wafugaji wameeleza namna BBT ilivyowahamisha kutoka ufugaji wa ufahari ya mifugo mingi, hadi wenye tija

"Najiona ni mmoja kati ya Wamasai wenye bahati sana, kuleta mabadiliko makubwa ya ufugaji katika familia na jamii yangu," anatamka Joyce Lemanda(28), akiendeleza ufafanuzi wake:

"Mwaka mmoja nyuma, kama nigeulizwa nitaweza kuleta mabadiliko gani katika familia yangu, nisingekuwa na jibu. Licha ya kusomea mifugo, sikuwa na ujanja huu kichwani mwangu"

Joyce anayetoka kijiji cha Lesoiti, Kata ya Lengatei, wilaya Kiteto, mkoani Manyara, anaiambia Nipashe namna mradi wa BBT ulivyobadilisha maisha ya familia yake na jamii katika ufugaji wa kisasa.

Akiwa mwenye shauku kuelezea mafanikio katika Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF), Joyce, anasema licha ya jamii yake kuwa na mifugo mingi, bado wapo katika umasikini, kwa sababu hawafugi kwa tija, wanaiweka zizini wakiamini kuwa na mifugo mingi ni sifa na jambo la kujivunia.

Joyce, mtaalamu wa mifugo katika ngazi ya cheti anasema, jambo hilo amekuwa akiona kasoro hiyo, akikiri alikwama katika maarifa ya mbadala wa kuchukuliwa, kubadilisha mtazamo wa jamii yake, hata ikaingia katika mabadiliko.

"Nilikuwa nikifika nyumbani nakuta tuna mifugo mingi zaidi ya 80, lakini bado tupo katika hali ya umasikini, mazingira pia yanaharibika. Ilikuwa inanisumbua sana akili, lakini sikujua kitu gani nifanye ili kuleta mabadiliko. Nilivyoona tangazo la kuomba kupata mafunzo haya ya BBT, nikajisemea 'Mkombozi huyu hapa'..." anasimulia Joyce

Joyce anaingia katika kundi la vijana takribani 240 nchini walionufaika na mafunzo ya mwaka mmoja ya kunenepesha ng'ombe, kaa, jongoo bahari na kilimo cha zao la mwani kwa vitendo chini ya mradi wa BBT - LIFE ili kufikia maono ya Rais Dk. Samia.

Hadi sasa, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, inaelekeza kutumia programu mbalimbali, zikiwamo za kilimo, mifugo na uvuvi, ili kujenga uchumi wa viwanda kupitia teknolojia na kuleta ushindani sokoni.

Joyce katika mazungumzo yake ambayo hakuchoka kila mara kumshukuru Rais Dk. Samia, kuwa na maono ya kuwapa fursa hiyo vijana, kwamba imebadilisha maisha ya familia yake.

Anasema katika mafunzo hayo walifundishwa ufugaji wa biashara, kwa maana ya kufuga na kuuza ili kupata mafanikio, jambo analokiri awali hakulifahamu, kwa kuwa ametoka katika jamiii yenye tabia ya "mifugo mingi ni sifa na heshima."

Mama wa kijana huyo anafafanua, walifundishwa namna ufugaji usio na tija ni adui wa mazingira, akiwa na ushuhuda wa kinachotokea nyumbani kwao, ardhi ikiathiriwa kwa kuwapo ng'ombe wengi katika eneo dogo.

Kwa mujibu wa Joyce, mradi huo- BBT, ulipompatia mafunzo ya namna ya kunenepesha mifugo kisasa, akayahamishia nyumbani kwao, hata akaona mafanikio, kwani ng'ombe wao wakanenepa kufikia kilo 400, kutoka kilo 200 za awali, jambo liliongezea thamani wakiwauza kwa bei inayofikia Sh. 600,000 kutoka Sh. 300, 000.

"Nyumbani kulikuwa na ng'ombe 80, mimi nikapewa 10 ku-


Inaendelea Uk. 13

AFYA

# Ukosefu wa uzio shuleni ulivyo mwanya bangi kuvutwa bwenini



Aliyekuwa Ofisa Elimu ya Sekondari Wilaya ya Longido, Gerson Mtera, alipozungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Ketumbeine, katika ziara yake shuleni hapo, Julai mwaka 2018. **PICHA: MTANDAO.**




**Na Zanura Mollel, LONGIDO**

MARA zote, dawa za kulevya inapozungumziwa, daima inaanza na dhana ya darasa endelevu katika maana yake. "Ni kilevi ambacho mtumiaji akishatumia, mfumo wa mwili na akili yake hubadilika, mtumiaji huweza kudhoofika kimwili au kupata madhara ya kiakili na baadhi huweza hata kufa..."

Hiyo inachukua sura, huku Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2015 (na mabadiliko ya 2017) inakataza kutumia, kusafirisha na kusambazwa dawa za kulevya,

Inadumu kuwa adha inayowaangukia hata baadhi ya wanafunzi bwenini katika shule za sekondari, ikiwamo mifano ya kunyooshewa mikono na Nipashe mkoani Arusha, shule zimekuwa zikipata kashfa wanafunzi kujihusisha na kutumia dawa za kulevya, hususani bangi.

Uchunguzi wa Nipashe umebaini, chanzo kikubwa ni kukosekana mazingira rafiki ya wanafunzi kujisomea, ikiwamo ukosefu wa uzio shuleni.

Kimsingi, uzio ni kizingiti kinachozuia kuingizwa dawa hizo katika mazingira yao na hasa bwenini, wilayani Longido kukiangukiwa na kashfa hizo.

Ni simulizi inayopata uthibitisho kutoka uongozi wa kishule na kiserikali, kunaibuka tabia ya wanafunzi kuingia na bangi shuleni kupita njia zisizo rasmi zinazokutana na miuundombinu ya shule wanayosoma.

Imebainika, baadhi ya wanafunzi wanaojihusisha na matumizi ya dawa za kulevya na kuna wakati wanaonekana kutoripoti shuleni pindi tu zinapofunguliwa, wakihofia ukaguzi kwa kishule kipindi hicho.

Ni aina ya tabia yenye ushuhuda wanafunzi hao huzunguka maeneo jirani na shule na kuna wakati wanaingia shuleni usiku kwa kupita 'njia za panya', lengo ni kupenya wakiwa na bangi au vilevi vingine vya siri, kama pombe.

Wanafunzi hao wanadaiwa wakificha bangi kwenye maeneo jirani na shule ambayo yamekuwa rafiki kwao, kisha wanafuata kuzichukua na wanatumia.

Aidha, simulizi zinadai wamefika mbali zaidi kuchimba mashimo maeneo ya shule yenye vichaka kidogo na kufukia, ili kuwapa urahisi kufikia muda atakaohitaji kutumia.

Lingine ni hali kwamba, wanaficha chini ya mawe katika mazingira ya maeneo ya shule, wengine wamefika mbali wakisaidiwa kuhifadhi na walinzi katika shule hizo.

Mwaka 2007, katika shule moja ya sekondari ndani Longido (jina tunalo), ambayo ni mchanganyiko wasichana na wavulana, walifukuzwa wanafunzi saba kwa kosa la kutumia bangi.

Mwaka 2021, pia katika shule nyingine ya sekondari wilayani Longido (nayo jina tunalo), nayo ikaingia katika historia wanafunzi kutumia bangi, huku mwezi uliopita, usiku wa kuamkia tarehe 25, wanafunzi 24 walikamatwa na walimu wao mwendo umbali wa saa kutoka bwenini, wakitumia dawa hizo.

Mkuu wa shule hiyo (jina tunalo), anasema katika kikao cha pamoja na wazazi wao, wakatambulika wanatoka katika maeneo maarufu kwa biashara, pia usambazaji bangi katika wilaya za Arumeru na Namanga.

UHALIFU UNAVYOFANYIKA

Inatajwa, siku wanayotumia dawa hizo, ni kuanzia Ijumaa hadi Jumapili, kutokana na kuwapo muda mrefu wa mapumziko, wengine wanajiunga na mafunzo ya 'skauti' ili wapate nafasi ya kwenda mafunzoni porini, kumbe wana azma mbadala.

Pia, shuleni wanatumia muda wa kupumzika jioni, wanaenda kuvuta bangi, huku utaratibu wa shule nyingi nchini sasa zimeachana na aina ya ukaguzi shuleni, maarufu 'rollcall.'

Kwanini dawa za kulevya? Imebainika kutoka taarifa ya kikao walikohojiwa wanafunzi hao katika shule mojawapo, ni dai kwamba inachangamsha akili zao, kuwawezesha kusoma muda mrefu, tofauti na wenzao wasiotumia

Nipashe imebaini hoja nyingine inatoka kwenye makundi wanayokutana nayo hasa nyakati za likizo wawapo majumbani, hasa panapokosekana usimamizi mzuri kwao, inawapa uhuru zaidi, pasipo nguvu ya usimamizi, kukiwapo wanaothubutu katika hatua ya kuuza bidhaa hizo.

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Longido, Atuganile Chisunga anafafanua "Mfano katika mpaka wa Namanga, wanafunzi wengi wa shule za msingi na sekondari, wamekuwa wahanga wa matukio haya, kutokana na hali ngumu ya maisha."

Anaendelea: "...wazazi kuwatelekeza na wengine kulelewa na mzazi mmoja, huku mzazi akizunguka kutafuta kazi kwa Wasomali za kufua na kufanya usafi, watoto wakitumika kuuza bangi na mirungi."

**HALI ILIVYO**

Katika video iliyofikia Nipashe, inaonyesha namna wanafunzi hao wameeleza katika kikao cha nidhamu kwamba, bila ya kutumia dawa hizo hawajihisi vizuri na wanapotumia hupata hamasa zaidi, mara nyingine wanalazimika kutafuta maji ya kunywa iwawezeshwe kuwa sawa, wenyewe huita 'arosto.'

Mwingine akakieleza kikao cha nidhamu kwamba anapokosa kuvuta bangi, analazimika kuhamia mbadala wa sigara. Pia, anapokuwa, nje ya shule akitumia bangi, kihisia anapendelea kukaa pekee yake, hapendi kuchangamana na watu.

Mmoja katika simulizi anasema, bangi inampa ujasiri kupimana nguvu na walimu wao, ila walifanikiwa kumdhibiti ipasavyo ikiwemo matumizi ya bakora.

Majumuisho ya kuwahoji 'wavuta bangi', wazazi wa wanafunzi hao walishirikishwa kwa kuhitajika kuwapokea makwao kwa wale wa vidato vya pili na nne, wakitakiwa kuja kipindi cha mitihani ya taifa pekee, lakini wa kidato cha tatu wazazi wakashauriwa kuwatafutia shule nyingine.

Hata hivyo, taarifa kutoka kikaoni zinaeleza wanafunzi wawili walikimbia kwenye usafiri waliokuwa wamepakiwa kwenda kukabidhiwa kwa wazazi wao.

Ni kashfa inayodaiwa, wanafunzi hao walikuwa wakitumia dawa,wakamfanyia ukatili mwanafunzi mmoja wao aliyewaona akalazimishwa kuvuta bangi, ikiwa sehemu ya kumdhibiti asitoe taarifa kwa walimu.

**KIONGOZI WA SHULE**

Joseph Kulunju , Mwenyekiti wa Bodi ya Shule ya Sekondari (jina tunalo), wilayani Longido, anakiri kuwapo tatizo la matumizi ya bangi kwa wanafunzi, huku akidai asilimia kubwa ya wanafunzi wanaokutwa na mkasa ni waliohamia kutoka shule nyinginezo.

Anasema, huwa wanapokea wanafunzi wahamiaji kutoka shule nyinginezo, lakini hawajui historia zao kama watumiaji wa dawa za kulevya, wakijiunga na shule hiyo ambayo katika bweni la wavulana, ina wanafunzi 80.

"Juzi tumesomewa mapato na matumizi, kiasi cha shilingi milioni 46 ni makusanyo ya watoto waliohamia na imesaidia kujenga bweni la wavulana," anasema Kulunju.

Hata hivyo, anawalaumu baadhi yao hatua inapochukuliwa dhidi ya watoto wao, wanakimbilia kwenye vyombo vya habari, badala ya kufika kupata taarifa sahihi na muhtasari wa vikao vyao.

Anafafanua haja ya kujengwa uzio wa shule, mwenyekiti wa bodi hiyo anasema kwa sasa kipaumbele, ni kujenga mabweni, akifafanua: "Hatuwezi kuanza ujenzi wa uzio huku tukiendelea kukabiliwa na changamoto ya bweni...tunategemea kupitia mahafali ya mwaka huu, kuwashirikisha wazazi juu ya umuhimu wa uzio."

**SAUTI ZA KISERIKALI**

Mbunge wa Longido ambaye pia ni Naibu Waziri, Dk. Steven Kiruswa, anatoa ombi kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya(DCEA), kuweka utaratibu wa kutoa elimu kwenye shule nchini itakayoambatana na sinema zenye kuonyesha athari ya dawa hizo, kwa lengo la kujenga hofu kwa wanafunzi kutumia.

Mwanasheria kutoka ofisi ya DCEA, Mseley Mfinanga, anafafanua kwamba anayethibitika kisheria kutumia au kujihusisha na uhalifu huo, huwa wanaadhibiwa kupitia Sheria ya Mtoto.

Atunganile Chisunga, Ofisa Ustawi Jamii wilayani Longido, anasema kupitia Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, inamlinda sana mtoto apatiwe elimu na kujiondoa kwenye matumizi ya dawa za kulevya.

Anasema matumizi ya bangi kwa wanafunzi katika shule za wilayani humo hajawahi kushirikishwa kiofisi, zaidi alishirikishwa matukio ya mimba pekee.

Pia, anazitaka mamlaka husika kuendelea kufuatilia zaidi kesi zinazoonekana kuripotiwa kwenye vyombo vya habari kuhusu dawa za kulevya na watoto.

"Watoto wengi ni waliohamia wanajihusisha na matumizi ya dawa hizo na hii inachangiwa na malezi na makuzi ya mtoto, wazazi hawana ushirikiano na walimu katika malezi.

"Baadhi ya sera nazo zimeonekana kuwapa ujasiri wanafunzi wakati mwingine kutaka kupigana na walimu," anatamka Chisunga.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido Simon Oitesoi, anasema Idara ya elimu Sekondari hajawahi kuwasilisha taarifa ya matukio ya matumizi ya dawa za kulevya shuleni, huku akidai matukio hayo hufanywa kwa siri na kutolewa maamuzi na bodi ya shule. Anamuagiza Ofisa Elimu kuiweka kwenye taarifa kwenye vikao vya halmashauri.

Ofisa Elimu Sekondari Halmashauri Longido, Gilbert Sombe, anaahidi kulifuatilia, hata kubaini undani wa madai ya mikasa hiyo ya wanafunzi kutumia bangi shuleni.

Kamishna wa Tiba na Kinga (DCEA), Dk. Peter Mfisi, anakiri kuwapo matumizi ya dawa za kulevya kwa wanafunzi hapa nchini na mamlaka hiyo imeanzisha vilabu vya kukabili matumizi ya dawa za kulevya (Anti_Drug Club) shuleni, kutoa elimu sahihi kwa vijana masomoni.

Aidha, Dk. Mfisi anasema wanatarajia kuanza kupima sampuli za mkojo kwa wanafunzi nchini, ikiwa sehemu ya kujiridhisha na nyendo zao dhidi ya dawa hizo, akitoa rai wanafunzi kutojihusisha na dawa hizo.

Kuhusu hatia za kisheria, anatamka: " Tutawafunga wangapi? Kikubwa ni kutoa elimu kwa jamii, pia kumfukuza shule mwanafunzi au kumpatia uhamisho bado tatizo litakuwa halijatatulika, kule anakohamia anakwenda kuongeza tatizo, kwa kuwafundisha wengine ambao walikuwa hawajui jambo hilo..."

AFYA

# Kliniki yaweka kambi ya kibingwa bure siku tatu, kurejeshea jamii shukurani

**Na Halfani Chusi**

NI kujali wagonjwa wake, pia kuunga mkono juhudi za serikali kwenye sekta ya afya, kliniki ya Kibingwa One Health Polyclinic iliyoko Kivule, Dar es Salaam, mwaka huu, kama ilivyo kila mwaka imeandaa kambi ya afya, huku umma wa wateja wake ukinufaika.

Ni kambi inayoitamka kuwa sehemu ya huduma kwa jamii ikitoa tiba bure au kwa punguzo maalumu kwa baadhi ya matibabu.

Mwaka jana kliniki hiyo iliweka kambi ya tiba kwa siku tatu mfululizo, kuanzia Tarehe 28 hadi 30 Januari, iliyoongozwa na kaulimbiu 'fahamu afya yako' ikilengea kuhimiza umuhimu wa kupima na kulinda afya.

Hiyo ni baada ya wao kubaini watu wanaweza kuishi na maradhi au kuwa na dalili hatarishi pasipo kujua na kushindwa kujikinga au kupata tiba kwa wakati.

Daktari Mfawidhi wa Kituo hicho Abel Nandonde, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mwendeshaji wa kituo, anasema lengo lao jingine lilikuwa ugunduzi wa magonjwa kwa wakati na kufuata mtindo bora wa maisha.

Anasema, kituo hicho kililenga kuwafikia wanajamii sita katika kambi hiyo, wakiwamo wanawake, wanaume, watoto na wazee. Kituo kwa mwaka huo, kilitekeleza azma hiyo kwa kushirikiana na wadau muhimu, anaowataja Ofisi ya Mganga Mkuu Jiji la Dar es Salaam, Mamlaka za serikali za mitaa kata za Kivule, Kitunda, Msongola na vituo vya afya jirani.

Anasema huduma za tiba na upimaji zilifanywa kwa ushirikiano na baadhi ya taasisi za serikali, akioongeza, ili kuweka tija na jambo lao kuwa la kipeke zaidi, kituo kilitenga ratiba mahususi ya ufunguzi rasmi ulioshirikisha viongozi mbalimbali pamoja na wananchi.

Anasema, baada ya tukio la ufunguzi, huduma kwa wagonjwa zilifanyika kwa siku tatu mfululizo na miongoni mwa huduma zilizotolewa siku hiyo ni pamoja na kuwaona madaktari bingwa bure.



Baadhi ya wauguzi, wa Kliniki ya One Health Poly Clinic wakimsadia mgonjwa aliyefika kwenye kambi ya matibabu bure. **PICHA: HALFANI CHUSI**

Pia, ikahusu kupatikana elimu ya Afya (juu ya kinga ya magonjwa, lishe, na usafi wa mazingira upimaji vipimo vya awali uzito, urefu na shinikizo la damu.

Huduma zingine zinatajwa ni upimaji wa awali wa kisukari, tezi dume, vilevile upimaji wa Virusi vya Ukimwi (VVU), utoaji wa chanjo ya korona, pamoja na vipimo vya mionzi ya sauti.

**MATOKEO YA KAMBI**

Daktari Mfawidhi Nandonde, anasema baada ya kambi hiyo, jumla ya wateja 515 walijiorodhesha kituoni kwao sawa na asilimia 86 ya lengo lao na kati yao, wateja 348 walifanyiwa vipimo vya uchunguzi wa afya ya awali, baadhi waligundulika kuwa na vihatarishi vya afya kama vile uzito uliozidi.

Anaongeza, pia waliweza kubaini changamoto kama vile shinikizo la juu la damu (high blood pressure) na upimaji dalili za awali za magonjwa yasiyoambukizwa, hali inayosaidia kuonyesha viashiria vya magonjwa ya kuambukiza, yaliyopo katika hatua za awali.

Kuhusu maradhi ya saratani, akasema upimaji wa saratani ya kizazi na matiti, ulifanywa kwa kushirikiana na wataalamu toka Taasisi ya Saratani ya Ocean Road.

Aliongeza, kuwa matokeo hayo yanaonyesha umuhimu wa kufanya upimaji wa afya kwa wakati, ili kuweza kugundua uwepo wa viashiria au magonjwa halisi na kupatiwa tiba mapema.

“Hivyo, kambi hii kupitia huduma bure na punguzo kubwa ya bei kwenye dawa na vipimo ilitoa fursa ya wananchi wengi kufaidika na huduma za vipimo vya mionzi, ambavyo pia vilisaidia wananchi kubaini baadhi ya changamoto ambazo zilihitaji vipimo hivyo kubainika.

'Vipimo vya 'ultrasound' viliwezesha kubaini magonjwa ya washiriki, jambo ambalo limekuwa lenye manufaa sana kwao,” anaeleza.

Anataja kwa siku hiyo, sampuli 221 zilichukuliwa kwa ajili ya vipimo vya maabara, na kutoa majibu mbalimbali. Vipimo vya maabara vilisaidia kubaini magonjwa ya mifumo mbalimbali ya mwili, ikiwamo njia ya mkojo na masuala ya uzazi.

Anaendelea na ufafanuzi kuwa sehemu kubwa ya wateja waliofika walifanikiwa kuonana na madaktari bingwa wa magonjwa ya ndani na magonjwa ya kinamama waliokuwapo, pamoja na timu ya madaktari wengine.

Tabibu huyo mfawidhi, anataja siku hiyo kituo kilitoa dawa bila ya malipo kwa baadhi ya wagonjwa waliokuwa na uhitaji mkubwa wakati wa kambi hiyo.

Huduma nyingine zilizotolewa, ni pamoja na huduma ya mashine za kupimia afya ukiwa nyumbani kwa ajili ya ufuatiliaji, zinazomuwezesha mgonjwa na mteja kutambua dalili za kudorora kwa afya, hata akaweza kuwasiliana na daktari kwa wakati.

Wateja pia, walipata fursa ya kupata baadhi ya huduma, kwa kulipia na kutoa maoni yao juu ya uboreshaji wa huduma za kituo.

“Matokeo haya ni mafanikio makubwa kwetu mwaka huu, pia tuna mpango wa kufanya hilo pamoja na washirika wetu, Uongozi wa One Health Polyclini na kampuni mama ya One Health Services. Tunaahidi kuendeleza utamaduni huu wa kutoa huduma kwa jamii, pamoja na kudumisha ushirikiano wetu na wadau,” anatamka. Anasema ni matarajio yao kupitia kambi hizo, wataendelea kuigusa jamii na kufanya maboresho ili iweze kuleta tija.

“Pamoja na kuwashukuru wadau ambao ni washirika wa kituo ikiwamo Halmashauri ya Jiji la Ilala (Dar es Salaa,), uongozi wa Kata ya Kivule na kata jirani, Serikali ya Mtaa wa Kerezange na mitaa inayozunguka kituo hicho”.

“Tunawashukuru wadau binafsi, zikiwamo kampuni za dawa, vituo vya kutoa huduma za afya vya jirani na taasisi za serikali zinazoshiriki nasi kuwafikia wananchi wa Kivule na kwingineko”.

“Kwa namna ya pekee kituo kinaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, kupitia Wizara ya Afya kwa kuendelea kutoa fursa kwa sekta binafsi kushiriki kuwahudumia wananchi” alisema.

## UTEKELEZAJI MRADI BBT ALIYOPIGIA MAKOFI RAIS '88', WANUFAIKA WAKE WATOA USHUHUDA

**INATOKA UK. 11**

toka kwenye mradi, nikawafundisha kunenepesha na kuuza. Hela tuliyopata, tukaongeza ng'ombe na sasa wapo 100. Kweli naona mabadiliko makubwa, kwani nyumbani kuna maendeleo, hapa pesa tunaiona na baba anawaza kujenga nyumba ya matofali kupitia mauzo, jambo ambalo halikuwapo hapo awali” anatoa ushuhuda Joyce.

Anasema, licha ya kwamba mafunzo anayopata hayajamalizika, wapo mwezi wa 10, tayari anaona mafanikio makubwa na malengo yake ni kubadilisha jamii yake iwe yenye kunufaika.

Mfugaji mwingine, Morianga Kasokwa (30), mkazi wa Lenguse-ro, Wilaya ya Kilindi, mkoani Tanga anasema elimu hiyo ya ufugaji wa kisasa au BBT, imemsaidia kubadilisha fikra ya familia na majirani zake, kutoka kufuga kwa ufahari hadi kibiashara.

Anasema ufugaji wa kifahari una madhara mengi kwa jamii yake, ikiwamo msongo wa mawazo kwa wamiliki, kwa sababu mifugo ni mingi inakutana na ugumu wa kuipatia malisho, hivyo waliumiza vichwa kupata malisho, huku kuna mabadiliko ya tabianchi.

“Hapo mwanzo baba yangu alikuwa ni mtu mwenye mawazo na hasira kila mara, muda wote alikuwa akilalamika ni wapi atapata malisho kwa n'gombe zaidi ya 100 aliokuwa nao, pia maisha yetu yalikuwa duni”

Anasema, baada ya mafunzo alimuweka mzazi wake chini na kumwelimisha kuwa anafuga kizamani, ufugaji usio na tija hivyo wakaanza kuuza ng'ombe na sasa wanafikiria ni biashara gani nyingine wafanye kupitia mauzo hayo.

Anasema kupitia programu hiyo wamefundishwa ujasiriamali na kuunganishwa na benki zinazotoa mikopo kwa wafugaji ikiwamo CRDB na sasa moja kati sababu zilizompeleka katika mkutano huo ni kuzungumza na maofisa wa benki hiyo kuona namna gani watawapa mkopo jamii yake ili kuboresha shughuli zao za ufugaji walifikie soko la dunia.

“Hapa unavyoniona nimekuja na maandiko yangu ya kibiashara kwa ajili ya kuyawasilisha kwa maofisa mikopo nione, na kuna benki kama TIB na African Development Bank tayari zimeonyesha nia, elimu ya kuandika maandiko ya mikopo nimepata kupitia programu ya BBT, kitu ambacho sikuwa nacho hapo awali, mawazo yangu yamefunguka sana kupitia programu hii na ninataka jamii yangu inufaike, ” anasimulia kwa kujiamini.

**WADAU WAKUU**

Akizungumzia mradi huo mkutanoni, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Ulega, anasema mwaka huu serikali imetoa shilingi bilioni 20.3 za utekelezaji mradi huo, kuongeza ushiriki wa vijana na wanawake katika sekta hiyo.

Mkurugenzi Mkazi wa Miradi wa Shirika la Heifer International, Mark, Tsoxo, anasema walishirikiana na serikali kuuandaa mradi huo ili ulete matokeo mazuri zaidi kwa vijana na wanawake.

# Serikali Yafanya kazi Saa 24 jijini Mwanza Kuongeza Majisafi kwa Wananchi

*Na mwandishi wetu.*




*Kazi ya ujenzi wa Dakio la Butimba na Kituo cha Kutibu Maji ikiendela katika jiji la Mwanza ambapo ujenzi wake umefikia hatua ya zaidi ya asilimia 90, hivyo kuleta tumaini la kukamilika na kuanza kuhudumia wananchi. Picha mashine ikitumika katika kazi ya kuunganisha bomba kubwa litakalotumika kuvuta maji kutoka maji ziwani.*

Serikali Yafanya kazi Saa 24 jijini Mwanza Kuongeza Majisafi kwa Wananchi

Kazi ya huduma ya maji kwa jamii ni baraka. Maji kwa hali yoyote ile hayana mmbadala wake. Kutokana na ukweli huu, Serikali nayo imeipa kipaumbele huduma ya maji kwa jamii ya Watanzania, waishio mijini na vijijini.

Ni saa 24 Serikali inaendelea kufanya kazi, usiku na mchana katika kuhakikisha huduma ya majisafi Jijini Mwanza na viunga vyake inaimarika zaidi na kuondosha mgao wa maji kwa wananchi. Mwanza ni jiji kubwa katika ukanda wa Afrika Mashariki kuendana na idadi ya watu na shughuli za kijamii ikiwamo viwanda, kilimo, biashara na idadi ya watu wanaoingia na kutoka kwa kazi mbalimbali za maendeleo.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) inahudumia jiji hili katika kusambaza huduma ya majisafi na salama kwa wananchi.

Hivi sasa jiji la Mwanza linahudumiwa na dakio la maji la Capripoint ambalo kwa mujibu wa takwimu lina uwezo wa kuzalisha lita za maji milioni 90 kwa siku, ila ukweli wa mambo kitaalamu kuendana na idadi ya watu na mahitaji ya huduma ya maji takwimu zinaonyesha kuwa mahitaji halisi ya maji ni zaidi ya lita milioni 160. Sensa ya mwaka 2022 inaonyesha jiji hili lina wakazi wapatao zaidi ya milioni 3.7.

Serikali imewasikia wananchi kuhusu maji, na Wizara ya Maji inafanyia kazi jambo hili ili kuleta utulivu kwa wananchi na kuwawezesha kutumia muda mwingi zaidi katika kufanikisha kazi za maendeleo na kuongeza thamani ya bidhaa mbalimbali kwa kutumia maji.

Hatua zinazochukuliwa katika kuleta utulivu hivi sasa ni pamoja na upanuzi wa dakio la maji la Capripoint. Kazi ya usanifu imefanyika na hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa katika kuhakikisha dakio hilo la Capripoint linakuwa na uwezo wa kuzalisha lita milioni 100 za maji kwa siku, hivyo kuongeza lita milioni 10 dhidi ya lita milioni 90 za sasa.

Mengine yanayofanyika ni ujenzi wa dakio jipya kabisa la Butimba na dakio jingine jipya la Igombe.

Kuhusu mradi wa dakio la Igombe Serikali inaendelea kujadiliana na Washirika wa Maendeleo ili kuweza kujenga dakio jipya hilo ambalo litazalisha lita milioni 200 kwa siku.

Mradi wa dakio la Butimba na kituo cha tiba ya maji uliopo wilaya ya Nyamagana umeshika kasi na muda sio mrefu kiu ya wananchi itatulizwa vya kutosha. Itakumbukwa kuwa mradi huu ulikaguliwa na kuwekewa jiwe la msingi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango tarehe 14 Septemba, 2022. Mkandarasi anayefanya kazi hii ni kampuni ya Sogea Satom, na thamani ya mradi ni zaidi ya shilingi bilioni 69, fedha ambayo imeshatolewa na Serikali.

Mradi huu utakaoleta mapinduzi makubwa katika Sekta ya Maji hususan katika jiji la Mwanza unafanikishwa kwa awamu mbili. Kwa kuzingatia hili, awamu ya kwanza ya ujenzi inayoendelea hivi sasa kwa nguvu kubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita, ambapo Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amenuia "Kumtua mama ndoo ya maji kichwani" inaenda kuzalisha lita milioni 48 na awamu iliyobaki itazalisha lita milioni 112, hivyo kufanya uzalishaji wa jumla ya lita milioni 160.

Kazi hii inasimamiwa kwa karibu na Serikali kupitia viongozi na wataalamu wake ambapo hadi muda huu utekelezaji wake umefika asilimia 94 ya ujenzi, na ukikamilika utanufaisha wakazi wa Mwanza wapatao zaidi ya laki nne na nusu.

Mradi utanufaisha wakazi wa maeneo ya Nyegezi, Mkolani, Buhongwa, Nyamazobe, Nyahingi, Buganda, Luchelele, Lwanhima, Sahwa, Fumagila, Kishiri na Igoma na kwa Misungwi ni Usagara, Nyashishi na Fella wakati kwa upande wa Magu ni Kisesa, Bujora na Isangijo. Wakazi wa maeneo haya wanatakiwa kujipanga kupata majisafi, salama na yenye kutosheleza kwa saa 24. Suala la mgao linaenda kuwa historia katika maeneo haya.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Mhe. Amina Makilagi akifanya ukaguzi wa mradi hii hivi karibuni amefurahishwa na kasi ya utekelezaji wake.

"Tunawashukuru na kuwapongeza MWAUWASA kwa utendaji wao wa kazi nzuri, kwa kipindi kifupi tumeona mabadiliko makubwa katika utekelezaji. Kwa kasi hii tunapata matumaini kwamba utekelezaji utakamilika ndani ya muda na huduma itapatikana kama ilivyokusudiwa," Mhe. Amina amesema baada ya kujionea hali halisi ya mradi.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Bi. Neli Msuya katika mahojiano maalumu amesema hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi ni ujenzi wa hatua za mwishoni.

"Hadi sasa kasi ya utekelezaji ni ya kuridhisha, sasa tunafanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha tunakamilisha kila hatua na tutafanya majaribio tarehe 15 Septemba, 2023 kama ilivyopangwa bila kukosa," Bi. Neli ameainisha.

Mradi wa Maji Butimba unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya na Shirika la Maendeleo la Ufaransa kwa gharama ya shilingi bilioni 69.

Kukamilika kwa mradi kutaboresha na kuwezesha upatikanaji huduma ya majisafi kwa wakazi wapatao 450,000 waishio maeneo ya pembezoni.

Ni wazi kuwa upungufu wa huduma hii muhimu ya maji inawagusa wananchi moja kwa moja, au kazi za kila siku wanazojihusisha nazo. Hilo ndilo limeisukuma Serikali kufanya kazi kwa saa 24 ili kuondosha uhaba huu katika baadhi ya maeneo, Pamoja na kwamba mgao wa maji unapunguza kiu ya wananchi. Hali ya huduma yam aji kwa wananchi inatofautiano kutoka eneo moja hadi jingine, hivyo hali hazilingani.

Asha Albinus wa Kishiri mkoani Mwanza anasema kuwa upatikanaji wa maji mwanzo ulikuwa wa shaka, ila kwasasa mgao umepunguza kiasi, mathitaji ya nyumbani yanapatikana kwa kiasi.

"Kwa sasa hivi ile shida kalis ana imepungua kidogo, ila kazi zaidi ifanyike maji yawepo kwa saa zote, tunahitaji maji, nawapongeza MWAUWASA kwa kujua hali zetu na mahitaji ya maji, watupe taarifa mapema pale kazi ya kusukuma maji inapokuwa na hitilafu ili tujiandae. Zaidi ya haya napongeza uongozi wa Awamu ya sita chini ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu kwa kubaini upungufu na tunaona mashine zikifanya kazi tupate maji" Bi. Edina Sendumba ambaye anaishi mtaa wa Mhandu jijini Mwanza anasema na kuongeza kuwa kama mama bila kuwa na maji kwa matumizi ya familia hawezi kuona kuwa amekamilisha majukumu yake nyumbani.

Mleshi Abdallah mkazi wa kata ya Kisesa anasema upungufu wa maji unawafanya akina mama kutembea mwendo kutafuta huduma hiyo, hivyo kusababisha adha kwa watoto, hasa kutoa huduma kwao kwani wanatakiwa kuwa na mama zao kwa muda mwingi.

Naye Salome Mango wa Igoma anasema kuwa kinachotakiwa ni uwepo wa maji muda wote ili kuondoa mawazo ya kutafuta maji au kuuziwa maji yasiyokuwa na uhakika wa ubora wake. Anatoa mwito kwa mamlaka

Mhe. Jumaa Aweso (Mb) hivi karibuni akiongea na Kamati ya Kuduma ya Bunge ya Maji na Mazingira amesema rasilimali za maji ni muhimu kwa maisha ya binadamu, ustawi wa jamii, maendeleo ya kiuchumi na uendelevu wa mazingira. Amesema maji ni msingi wa maendeleo na yanahusiana na sekta nyingine ambazo ni pamoja na nishati, viwanda, kilimo, uvuvi, mifugo, madini, maliasili na utalii. Hivyo maji ni chachu na muhimu kwa kila jambo na maendeleo.

"Tunafanya kazi kama timu katika kutoa majibu kuhusu huduma ya maji, kuanzia wataalamu wafanyakazi katika Sekta ya Maji na sisi viongozi" Mhe. Aweso anasema na kuongeza changamoto ya wananchi hatutaki kuizoea, tupo ili kuwapa wananchi suluhu, na tunafanya kazi usiku na mchana.

Ameongeza kuwa Chuo cha Maji kilichoanzishwa mwaka 1974 kinatumika kuongeza nguvu kazi inayotumika katika Sekta ya Maji, nguvu kazi yenye ujuzi, weledi na umahiri katika Sekta ya Maji ili kuleta suluhisho katika huduma ya maji kwa Watanzania.

Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akihutubia Bunge mwezi Aprili 2021 alisema "katika miaka hii mitano, tutaweka mkazo mkubwa katika kuimarisha usimamizi kwenye utekelezaji wa miradi ya maji. Lengo letu ni kufikia azma ya kufikisha maji kwa wananchi kwa asilimia 95 mijini na asilimia 85 vijiji ifikapo mwaka 2025".

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Amos Makala akiongea hivi karibuni kuhusu mradi huu ametaka mkandarasi awajibike katika kuwapatia wananchi huduma ya maji, na asiwe na sababu kwani suala la fedha Serikali imempatia ili afanye kazi kwa haraka.

Kwa muktadha huu, lengo la Serikali ni kuhakikisha huduma ya maji kwa wananchi, mijini na vijijini inaimarika. Kazi za miradi mipya na uboreshaji wa miradi inayoendelea jijini Mwanza ni suluhu ya uhaba wa maji kwa wakazi na shughuli mbalimbali wanazofanya ili kujiletea maendeleo na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Wataalamu wa masuala ya maji katika maandiko mbalimbali wanasisitiza utunzaji na uendelezaji wa vyanzo vya maji ni muhimu sana ili miradi ya maji inayojengwa na Serikali kwa kutumia fedha nyingi iwe endelevu. Moja ya katazo ni kukoma kwa shughuli za kibinadamu katika vyanzo vya maji ili rasilimali hii muhimu isipotee na kupoteza utulivu kwa jamii yetu na majirani pia. Wananchi ndio walinzi wakuu wa vyanzo vya maji na ushirikishwaji wao katika ulinzi ni jambo la msingi.

Tafiti iliyofanywa na Mahendra, A (2021) pamoja na wenzie kuhusu Maji na Mabadiliko Mijini; Changamoto za Afrika anasema kuwa miji katika bara la Afrika inapata changamoto ya huduma ya maji kwa sababu anuai ikiwamo mabadiliko ya tabianchi, kukua kwa miji na idadi ya watu hivyo kutishia uchumi, maisha na afya ya wakazi wake.

Kutibu haya, Mahendra katika utafiti huo anasema kuwa ili kuepuka matokeo hasi, vyanzo vya maji lazima vitunzwe ili kuhimili majanga ya asili. Pia, kuimarisha uwekezaji katika eneo la maji. Pamoja na mengine, kuhusisha taasisi mbalimbali za ubunifu na kuongeza ushirikishwaji wa wadau katika kulinda rasilimali za maji.

Hivyo, moja ya hatua ya msingi ni kuhifadhi na kuendeleza vyanzo vya maji, kuwa ni jukumu la kila mwananchi. Uharibidu wa vyanzo vya maji matokeo yake ni mabaya, shughuli za kilimo katika vyanzo vya maji hazifai, ni kuamini kuwa "Jibini haiwezi kuyeyuka ikiwa mdomoni", jambo ambalo sio kweli. Kila mwananchi awajibike kwa kuwa mlinzi katika jambo hili muhimu.

Afrika imetia saini mikataba kadhaa ya kimataifa kama vile wa Kyoto na makubaliano ya Paris ya 2015 kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi. Makubaliano haya ya kimataifa yanalenga kupambana na kurudisha nyuma athari za mabadiliko ya tabianchi.

Athari kubwa katika hili zilionekana wakati kimbunga Idai kilipozikumba nchi za kusini mwa Afrika za Msumbiji, Zimbabwe na Malawi. Ni Kumbukumbu isyivutia kuwa Afrika inabaki kuwa bara lililoko hatarini kwa kadri suala la kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi linavyohusika.

Utafiti wa Asasi ya Afrobarometer (2019) umeonyesha kuwa mazingira ya kilimo yanazidi kuwa mabaya kutokana na mvua zisizotabirika, ubora wa maisha kupungua na maarifa kidogo au kutokuwepo kabisaa kwa ufahamu kuhusu madhara ya mabaliko ya tabianchi.

Ni jambo la msingi wananchi kuwa walinzi katika kulinda na kuhifadhi rasilimali za maji ili kuepuka majanga ambayo yanakuwa nje ya uwezo. Haya ni maarifa ambayo yapo wazi, jamii ishirikishwe kupata maarifa zaidi kuepuka uharibifu wa vyanzo vya maji.





# RC azionya halmashauri zinazotumia mashine feki

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ameziagiza halmashauri kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kuonya watakaobainika kutumia mashine za kukusanya fedha (POS) feki watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Serukamba alitoa maagizo hayo jana kwenye kikao kazi cha wakurugenzi, wakuu wa wilaya, wenyeviti wa halmashauri na wataalam mbalimbali kilichofanyika mjini hapa.

Alisema kumekuwa na tatizo la ukusanyaji wa mapato na matumizi ya POS feki na hivyo kuukosesha mkoa kupata mapato stahiki.

"Naomba vyombo vya dola ikiwamo na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kusaidia kufanya uchunguzi kwenye mageti ya ukaguzi wa mazao yanayosafirishwa," alisema.

Serukamba alisema Mkoa wa Singida unaweza ukawa kinara wa ukusanyaji wa mapato, uhifadhi wa mazingira na usimamizi wa miradi iwapo watendaji watafanya kazi kwa kujituma na kushirikiana badala ya kuyaachia baadhi ya makundi kufanya kazi hizo.

"Tukifanya kazi vizuri katika uhifadhi wa mazingira, ukusanyaji mapato, ukamilishaji wa miradi kwa wakati na kuwa timu moja, siku moja tutakuwa namba moja kitaifa," alisema Serukamba.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk.Fatuma Mganga akizungumza kwenye kikao hicho aliwaomba wakurugenzi pindi wanapopokea fedha za miradi kabla ya kuanza kutekeleza watoke ofisini na kwenda kujua bei za vifaa badala ya kuwaachia watu wa manunuzi pekee ambao wamekuwa na tatizo la kuweka bei ya juu.

"Miradi mingi imekuwa haikamiliki kutokana na fedha zilizotolewa na serikali kumalizika kabla haijaisha na hiyo inasabisha kununua vifaa kwa bei kubwa lakini wakurugenzi wakitoka na timu yao watawakuta wauzaji wa vifaa hivyo kwa bei ya chini," alisema.

Akitolea mfano alisema alipokuwa Mkurugenzi wa Halmashauri wakati wanataka kutengeneza milango waliwaomba watu wa manunuzi wawape bei yao na wakasema ni Sh.milioni 72 lakini walipotoka kutafuta bei kwa watu wengine kulikuwa na kati ya Sh.milioni 48 hadi Sh. milioni 50 na waliamua kuitoa kazi kwa mwenye bei ya chini.

Dk. Mganga aliwaomba wakurugenzi hao kujenga tabia ya kwenda kujifunza kwa wenzao ambao wanatakiwa kukamilisha miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa fedha zilezile walizopokea kama wao.

Alisema: "Utakuta serikali imetoa fedha kiwango sawa lakini katika ukamilishaji wa miradi kwa fedha hizo hizo halmashauri zingine zinakamilisha miradi iwe ya ujenzi wa shule au kituo cha afya na halmashauri nyingine utakuta ujenzi wake upo hatua ya msingi".

# Walimu Hisabati wajengewa uwezo kuongeza ufaulu

**Na Elisante John,** IRAMBA

SERIKALI imeanza kuwajengea uwezo viongozi wa elimu na walimu wa somo la Hisabati wilayani Iramba mkoani Singida kutokana na wilaya hiyo kufanya vibaya kwenye mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2022.

Hatua hiyo imetokana na matokeo ya mtihani huo kuonyesha kiwango cha ufaulu somo la hisabati kipo chini ya asilimia 34, ikiwa ni cha chini zaidi, kuliko halmashauri zingine sita za Mkoa wa Singida.

Mratibu Msaidizi, Programu ya Shule Bora kutoka Taasisi ya Elimu nchini (TET), Mwesiga Kabigumila, alisema mafunzo hayo yanahusisha walimu wa shule za msingi 50 wa somo la hisabati, waratibu kata 10, walimu wakuu 20 na viongozi wa ngazi mbalimbali wa wilaya hiyo.

Alibainisha kuwa mafunzo hayo yana lengo la kuboresha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ili kuondoa vikwazo vya walimu wanaofundisha somo hilo. Hivyo, aliwataka walimu hao kuyaelewa mazingira ya wanafunzi wanaowafundisha sambamba na kutengeneza zana zinazotoka kwenye maeneo yao halisi, kwa ajili ya kuboresha na kusaidia ufundishaji na ujifunzaji kwa somo la hisabati.

Naye, Kaimu Ofisa Elimu wa Mkoa wa Singida, Sarah Mkumbo, alitumia fursa hiyo kuwataka washiriki wazingatie mafunzo hayo, ili mbinu wanazopewa zilete tija katika somo hilo kwa kuongeza ufaulu.

Mkumbo alifafanua kuwa pamoja na kazi nzuri inayofanywa na uthibiti ubora katika kutekeleza majukumu ya kuwasimamia walimu, lakini mafunzo hayo yatawajengea uwezo na kuwaongezea maarifa zaidi, kwa ajili ya ufundishaji wao darasani.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akisalimiana na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, walipokutana Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bado Watanzania 9,052,174 kupata vitambulisho vya taifa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa hadi kufikia Julai 31 mwaka huu Watanzania 11,242,736 wamepewa vitambulisho vya taifa sawa na asilimia 55 ya lengo la kuwapatia wananchi 20,294,910 wanaostahili kupewa.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Khamis Hamza Khamis alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti maalum (CHADEMA), Esther Matiko kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Katika swali lake, mbunge huyo alitaka kujua asilimia ngapi ya Watanzania wameandikishwa na kupatiwa kitambulisho cha taifa.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema mpango wa serikali ni kuwagawia vitambulisho Watanzania 9,052,174 waliobaki ifikapo Machi, 2024.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Grace Tendega, alihoji kwanini serikali inachukua muda mrefu kutoa vitambulisho hivyo kwa Watanzania kwa kuwa inawakosesha fursa mbalimbali.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema serikali haijachukua muda mrefu kutoa vitambulisho na kwamba hapo awali kulikuwa na tatizo la upungufu wa vitambulisho vilivyokuwa vinatoa vitambulisho kwa kasi. "Kwasasa tumepata mashine bora za kisasa na tutahakikisha Watanzania wote wanapata vitambulisho ili kupata huduma," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali imeona kuna haja ya kuunganisha kitambulisho hicho kuwa na taarifa zote muhimu ikiwamo za kibenki na ipo mbioni kushughulikia suala hilo.

# Hospitali, vituo vya afya vya makanisa kuboreshwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Kikristo ya Huduma za Jamii (CSSC) imetaja mikakati yake ya kuzijengea uwezo hospitali na vituo vya afya vinavyomilikiwa na makanisa, ili kutoa huduma bora za afya kwa wananchi.

Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka jana makanisa yanaendesha vituo 900 vya huduma za afya ikiwamo hospitali 105.

Mratibu wa Ubora kutoka CSSC, Dk. David Isaya aliyasema hayo jana kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa Chama Cha Madaktari Wakikristo Tanzania (TCMA).

Alisema mikakati hiyo ni kuwaunganisha watoa huduma za afya kwenye hospitali na wengine ili kubadilishana uzoefu unaolenga kuimarisha utoaji huduma bora za afya.

"Miongoni mwa changamoto inayozikabili hospitali na vituo vya afya ni rasilimali fedha na watu katika sekta ya afya, tumechukua hatua kwa kuimarisha mifumo ya uongozi thabiti na kuzijengea uwezo menejimenti za hospitali pamoja na utoaji wa vitendea kazi," alisema.

Alisema mbinu wanazotumia kuboresha huduma ni kuwa na watu sahihi kwenye vitengo husika na matumizi ya miongozo sahihi katika kutoa huduma za afya.

Naye, Mganga Mfawidhi katika Hospitali ya St. Joseph mkoani Kilimanjaro, Sista Dk. Hellen Benedict, amesema wamejifunza mambo mbalimbali ambayo yanahusika na uwajibikaji na utoaji wa huduma bora.







Mfanyabiashara wa viazi mviringo (kulia), akiwahudumia wateja wake katika eneo la Lungemba, wilayani Mufindi mkoani Iringa jana. Debe moja la viazi liliuzwa kwa 10,000/-. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mgombea ubunge alalamika picha zake kunyofolewa

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

MGOMBEA ubunge Mbarali mkoani Mbeya kupitia Chama cha ADC, Innocent Siliwa, amelalamikia wanachama wa baadhi ya vyama vinavyoshiriki uchaguzi huo kuanza kumhujumu kwa kubandua mabango yake kwenye baadhi ya maeneo.

Siliwa alitoa malalamiko hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari ambapo alisema katika baadhi ya maeneo watu hao waliondoa hata bendera za chama chake jambo ambalo alisema halitakiwi kwa mujibu wa sheria za uchaguzi.

Alisema katika kufuatilia alibaini kuwa wanaoondoa mabango hayo ni makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na hivyo akatoa taarifa na wakasuluhishwa jambo hilo likaisha lakini bado linaendelea kwenye maeneo mengine.

Aliyataja maeneo ambayo mabango yake yaliondolewa kuwa ni katika vijiji vya Igava, Manienga na Igunda na kwamba walipofuatilia walibaini kuwa mabango ya CCM ndiyo yaliyobakia kwenye maeneo hayo. "Tulisuluhishana na wakarejesha bendera yetu japo iliwekwa kwenye mlingoti ambao siyo sahihi kabisa, hili tunaomba msimamizi wa uchaguzi alifahamu kabisa kwamba tunafanyiwa uhuni huo," alisema Siliwa.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbarali, Mary Mbwilo, alikana chama chake kuondoa mabango ya mgombea yeyote huku akidai kuwa mgombea wa ADC hakuna mahali popote alipobandika mabango.

Alisema yeye pamoja na timu yake wamezunguka katika kata zote za wilaya hiyo na hakuna mahali ambapo waliona bango la Siliwa na hivyo akamtaka aache uongo.

Alisema walishakubaliana kwenye vikao kwamba zinatakiwa kufanyika kampeni za kistaarabu na hivyo anashangaa kusikia mgombea huyo akilalamika kuwa anafanyiwa hujuma.

Msimamizi wa uchaguzi wa Mbarali, Misana Kwangula, alikiri kupokea malalamiko ya Siliwa na kwamba alitoa malalamiko hayo kwa mdomo wakamtaka awasilishe kwa mandishi lakini hakutekeleza mpaka sasa.

Alisema kwa mujibu wa sheria na kanuni za Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni kwamba malalamiko ambayo yanashughulikiwa ni yale ambayo yanawasilishwa kwa njia ya maandishi na siyo kwa mdomo.

"Nilikuwa niko safari nikampa maelekezo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wa Jimbo ampe maelekezo mlalamikaji alete maandishi lakini mpaka narejea alikuwa hajatekeleza na mpaka sasa hajafanya hivyo, sasa hatuwezi kufanyia kazi maneno," alisema Kwangula. Alisema ipo Kamati ya Maadili ambayo kazi yake ni kushughulikia migogoro ya aina hiyo lakini inashughulikia mgogoro ambao umetolewa taarifa ya maandishi.

Uchaguzi mdogo Mbarali unatarajiwa kufanyika Septemba 19 mwaka huu na unafanyika kwa lengo la kuziba pengo lililoachwa na Francis Mtega ambaye alifariki baada ya kugongwa na trekta alipokuwa anaendesha pikipiki kwenda shambani.

# 'Wazazi waleteni shuleni watoto waliopata ujauzito'

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAZAZI na walezi mkoani Njombe wametakiwa kurejesha shuleni wasichana waliokatishwa masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo mimba, kupitia mradi wa Sequip na siyo kuwatumikisha kiuchumi.

Wito huo ulitolewa na Mkufunzi Mkazi wa Mkoa wa Njombe, Alto Mbena, wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake ambapo alisema ni wakati wa wazazi kuamka kuitumia nafasi hiyo ili kuwasaidia watoto wa kike kupata elimu.

"Serikali imetoa fedha nyingi ili kufanikisha na hilo siyo Njombe tu maana yake ni kwa nchi nzima, mimi nadhani ni wakati wa wazazi kuamka na kuwasaidia wanafunzi ambao wamepata mimba bahati mbaya shuleni basi wananafasi ya kujiuliza tena"alisema Mbena.

Alisema serikali imetoa fursa kwa wanafunzi wa kike kurudi darasani na kusoma bure.

"Mzazi unagharamia tu nguo zake mtoto lakini suala la ada ya shule sujui na nini halipi chochote, ada ya mtihani halipi chochote unaona ni fursa ambayo ni adimu kupatikana lakini kwetu imewezekana, serikali imeliwezesha hilo sasa mzazi unapokwama kumpeleka mwanafunzi shuleni yani tu kwa sababu umeshazoea kumtumia kama kitega uchumi yani yeye akatafute fedha upate kula mimi nawashauri kwamba wasifanye hivyo"alifafanua Mbena.

Aliongeza: "Mwaka jana wakati natafuta wanafunzi kuna mzazi alimshikilia mtoto kwamba hataenda shule kwa sababu wanamtumia kama kitega uchumi, mimi nilichokifanya nikamwambia nitakuletea polisi akatishika alimleta yule mtoto na anasoma" alisema.

Hata hivyo aliwataka wananchi wa Njombe kutumia fursa ambayo Rais Samia ameitoa ya kuhakikisha mtoto wa kike anapata elimu licha ya changamoto.

"Wananchi wa Njombe waone umuhimu wa kutumia hii fursa kwa sababu fedha nyingi inatumika, hela nyingi na hii fedha serikali inatoa kwa malengo ya kuifanya jamii yake iweze kupata elimu, sasa mzazi anaona fedha inatumika alafu badala yake unamtumia mtoto kama kitega uchumi hilo ni tatizo nawaomba wawalete shuleni"alisema Mbena.

Mbena alibainisha kuwa: "Hata kama mzazi anayo shughuli ya kumpa mtoto lakini hana elimu bado hujamsaidia kwa sababu hizo mali au fedha ambazo zipo za kumuwezesha mtoto mimi nafikiri ni vizuri ukamuwezesha kwenye elimu ili baadae aweze kujitegemea mwenyewe, pengine mzazi kajenga chuki kwa mtoto kwanini kapata mimba alafu ukamsusa ukaona hana sababu ya kusomeshwa ni jambo ambalo sio sawa" alisema.

Wakizungumza na Nipashe mmoja wa wakazi mjini Njombe amewatupia lawama wazazi ambao wameshindwa kuwapeleka watoto wao shule licha ya serikali kutoa fursa.

Asifiwe Mwalongo alisema "Urithi wa mtoto ni elimu haijalishi awe wa kike au wa kiume, mtoto anapokosea jaribu kumpa nafasi ya pili kwa sababu serikali iliona tatizo liko wapi ndiyo maana wakaja na huu mpango, tupeleke watoto wa kike shule tuache visingizio".

# Wafugaji wakoshwa uanzishwaji Jukwaa la Wanawake Vijijini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAWAKE jamii ya wafugaji wa kabila la masai wamesema Jukwaa la Wanawake wa Vijijini lililoanzishwa hivi karibuni ni fursa inayopaswa kutumika kuwakomboa wanawake wa jamii za kifugaji kutokana na matatizo mbalimbali ambayo yanawakabili.

Waliyasema hayo walipozungumza na Nipashe jijini Mbeya baada ya kuanzishwa kwa jukwaa hilo Tawi la Tanzania ambapo walisema moja kati ya matatizo ambayo yamekuwa yakiwakabili ni pamoja na kukosa haki ya kumiliki rasilimali.

Walizitaja rasilimali ambazo wananyimwa haki ya kumiliki kuwa ni ardhi pamoja na mifugo licha ya kuwa wao ndio wazalishaji katika familia zao.

Mmoja wa wanawake hao, Eloy Satulo, kutoka Kijiji cha Matebete kilichopo katika Kata ya Itamboleo wilayani Mbarali, alisema bado juhudi za ziada zinahitajika ili kumuweka huru mwanamke wa kimasai na jamii nyingine za wafugaji.

Alisema kwenye maeneo yao mali nyingi zinazalishwa kwa ushirikiano kati yao na waume zao na zingine wanazalisha wao lakini umiliki wote unakuwa kwa mwanamme.

"Tatizo kubwa ni kuwa wanawake katika jamii za kifugaji hasa kwa sisi wamasai wengi hatumiliki rasilimali, hiyo mifugo tunayofuga ni miliki ya wanaume, maana yake hata kwenye familia akiitwa huyu ng'ombe ni wa kwako inabakia ni jina tu," alisema Eloy.

Alisema pamoja na juhudi zinazofanywa na serikali kwa kusaidiana na wadau mbalimbali katika kumkomboa mwanamke bado kuna vikwazo.

Naye Truket Akasho, mkazi wa Kijiji cha Mwanavala Kata ya Imalilo Songwe wilayani Mbarali alisema jukwaa hilo litakuwa chachu na lenye msaada kwa wanawake vijijini iwapo kazi zake zitajikita maeneo ya pembezoni kama ilivyo malengo yake.

Truket ambaye pia ni Diwani wa Viti Maalumu wilayani Mbarali alisema atahakikisha jukwaa hilo linafika hadi katika vijiji vinavyomzunguka.

"Mimi nimefika hapa kama mwakilishi wao nitapeleka huu ujumbe, tuna majukwaa kijijini na nina vikundi vya wanawake wenzangu ambavyo nimekuwa nikifanya navyo kazi vijijini, kupitia vikundi hivyo wanawake wananufaika kupitia ujasiriamali," alisema Truket.

Alisema kuna migogoro mingi ya ardhi ukiwemo mgogoro baina yao na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha akidai kuwa mpaka mpya umesababisha maeneo yao mengi yachukuliwe na hifadhi na hivyo akasisitiza kuwa watahakikisha wanatoa elimu kwa wenzao kumiliki maeneo yao kisheria.

Jukwaa la Wanawake Vijijini kwa mataifa mengine yaliyopo Ukanda wa Kusini mwa Afrika yaani nchi za SADC lilishiriki uzinduzi wa jukwaa hilo ambalo kwenye baadhi ya mataifa lilikuwa limeshaanzishwa.

Aidha, jukwaa hilo linalenga kuwezesha wanawake kujikita katika agenda muhimu za ardhi, kilimo ikolojia, ukatili wa kijinsia na mabadiliko ya tabianchi kwa kuwajengea uwezo katika maeneo hayo.



# ‘Viongozi vyama vya siasa msiwazuie wanawake kujieleza’

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

VIONGOZI wa vyama vya siasa wametakiwa kuwaruhusu wanachama wao wanawake kutumia haki zao za kujieleza katika maeneo yao ya kazi, ili kuimarisha utendaji na hali zao.

Ushauri huo umetolewa jana na Kamati ya Wataalamu wa Masuala ya Habari Zanzibar (ZAMECO) wakati wakitoa taarifa kwa vyombo vya habari.

Kamati hiyo imehusisha Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA Zanzibar), Baraza la Habari Tanzania (MCT), Jumuiya ya Waandishi wa Habari za Maendeleo Zanzibar (WAHAMAZA), na Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC).

Taarifa hiyo imekuja ikiwa ni siku chache tangu Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuteua na kuwaapisha wajumbe saba wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar ambayo ina wanawake wawili.

Taarifa hiyo ilisema katika tamko hilo limekuja baada ya tukio la mjumbe mmoja wa wanawake hao kukataa kutoa maoni yake binafsi baada ya hafla ya uapisho, licha ya kuwa awali alikubali vizuri.

“Inasemekana kuwa uongozi wa chama chake ulimzuia mjumbe huyo mwanamke kuzungumza ili kueleza hisia zake kuhusu kuteuliwa kwa mara ya kwanza kuwa Kamishna wa Tume ya Uchaguzi” ilisema taarifa hiyo.

Aidha, taarifa hiyo ilisema huwa ni kawaida kwa waandishi wa habari kufanya mahojiano baada ya viongozi kuapishwa ili kuelezea hisia zao na wajibu wao kwa wananchi, hivyo mteule huyo alitegemewa na yeye kutumia nafasi hiyo.

“Kutoa maoni yake ni suala la haki yake ya msingi kwa ubinaadamu wake na sio kuhusiana na chama atokacho; hivyo haikustahili na si katika jambo jema kumzuia hasa kama mwenyewe alikuwa tayari kuzungumza na waandishi wa habari” ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa matokeo ya kadhia hiyo ni kwamba habari zilizotoka kuhusiana na tume hiyo zilikosa sauti za wanawake, hivyo kuendeleza mfumo dume wa wanaume kutawala katika vyombo vya maamuzi na vyombo vya Habari.

Katika kikao chake cha hivi karibuni, mashirika hayo ya habari pamoja na waandishi wa habari pamoja na mambo mengine, walizungumzia tukio hilo na kueleza kusikitishwa na kitendo hicho cha kumkosesha mwanasiasa mwanamke kujieleza mbele ya waandishi wa habari.

Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Ibara ya 18. (1) inaelekeza kwamba “... bila ya kuathiri sheria za nchi, kila mtu yuko huru kuwa na maoni yoyote na kutoa nje mawazo yake na kutafuta, kupokea na kutoa habari na dhana kupitia chombo chochote, bila ya kujali mipaka ya nchi na pia ana uhuru wa mawasiliano yake kutoingiliwa kati.”




Baadhi ya waandishi wa habari wanawake Zanzibar, wakipatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya mitandao kidigitali yaliyotolewa na Taasisi ya Zaina Foundation Tanzania, Unguja juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZIPA yawaita wawekezaji kuwekeza Mangapwani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), Sharif Ali Sharif, amewataka wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kujitokeza kuwekeza katika sekta ya mafuta na gesi.

Amesema Serikali ya Zanzibar imetenga eneo la Mangapwani kwa uwekezaji huo wenye ukubwa wa hekari 933.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, alisema serikali imetenga eneo hilo kwa ajili ya uwekezaji wa mafuta na gesi, ujenzi wa nyumba za makazi na ujenzi wa mji mpya katika eneo hilo.

“Eneo lilotengwa kwa ajili ya uwekezaji wa maguta na gesi pekee lina ukubwa wa hekari 47.57 hivyo ni vyema wawekezaji kujitokeza kuwekeza katika sekta hiyo” alisema.

Aidha, alisema eneo la Mangapwani linakusudiwa kufanywa kuwa moja katika maeneo ya kiuchumi kwa kuanza na kutangazia fursa za upatikanaji wa maeneo ya uwekezaji wa mafuta na gesi pamoja na mfumo wa ushushaji mafuta kutoka katika meli hadi katika tangi.

Alisema hatua hiyo itaweza kuhudumia wawekezaji wote watakaokuwepo katika eneo hilo kwa upande wa sekta ya nishati hiyo.

Sharif alisema eneo hilo limegaiwa katika maeneo makuu matatu ikiwemo eneo la kwanza ambalo lina ukubwa wa hekari 17.8, eneo la pili linaukubwa wa hekari 16.2 na eneo la tatu linaukubwa wa hekari 13.56.

Hata hivyo, alisema maamuzi ya kutangazia fursa hizo za uwekezaji ni mwendelezo wa juhudi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuleta maendeleo, kukuza uchumi wa nchi ambao utamgusa mwananchi moja kwa moja.

# Marais nchi saba kujadiliana kuhusu mifumo ya chakula

**Na Restuta James**

MARAIS saba kutoka Afrika wamethibitisha kushiriki majadiliano na kisha kuja na makubaliano ya kuimarisha mifumo ya chakula, kwenye mkutano maalumu utakaofanyika jijini Dar es Salaam leo.

Kabla ya kufanyika kwa mkutano huo, Rais Samia Suluhu Hassan, atawahutubia vijana wa Afrika wanaojihusisha na kilimo na wale waliopo kwenye mnyororo wa thamani wa bidhaa za kilimo.

Akizungumza na waandishi jana, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema wakuu hao wa nchi watashiriki majadiliano ya Jukwaa la Mifumo ya Chakula (AGRF), linaloendelea jijini hapa.

Kongamano la AGRF lilianza Septemba 5 na litahitimishwa Septemba 8, mwaka huu.

Msigwa alisema baadhi ya nchi marais wametuma wawakilishi na wengine wanaendelea kuthibitisha kulingana na taratibu za kiusalama.

Kabla ya majadiliano hayo ya marais, Rais Samia Suluhu Hassan, atahutubia vijana wa Afrika wanaojishughulisha na kilimo.

“Marais waliothibitisha kushiriki ni saba, wengine wataendelea kuthibitisha kwa sababu mkutano ni kesho (leo), inawezekana wakaongezeka au wakaja kwa uwakilishi,” alisema Msigwa.

Msigwa alisema kila rais atatoa hotuba yake watapokea taarifa mbalimbali na kutoa maazimio ya mkutano.

“Kesho hiyo jioni Rais Samia amealika wageni Ikulu ambapo tuzo ya mzalishaji bora wa Chakula Afrika itatolewa,” alisema.

Kuhusu vijana, Msigwa alisema Rais Samia atapokea taarifa juu ya namna vijana wa Afrika wanajihusisha na kilimo na kutumia fursa mbalimbali zinazopatikana kwenye sekta hiyo.

“Baada ya taarifa hiyo na yeye atatoa mwelekeo wake juu ya namna anavyoona Bara la Afrika linavyoweza kusaidia vijana kupata ajira kupitia kilimo,” alisema Msigwa.

Akizungumzia jukwaa la AGRF, Msigwa alisema mkutano huo umewakutanisha wadau wa kitaifa na kimataifa, kutoka ndani na nje ya Bara la Afrika.

“Kwa upande wa Tanzania, serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika sekta hii na sasa bajeti inakaribia Sh. trilioni moja ili kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo kwa lengo la kuwatoa wakulima katika kilimo cha mazoea cha kutegemea mvua,” amesema Msigwa.

Alisema lengo lingine ni kuwasaidia wakulima kupata mbegu bora, kuwa na hifadhi nzuri ya mazao na kuhamasisha vijana wajishughulishe kwenye kilimo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**LILIAN ALLEN MMARI**

MTAJWA HAPO JUU AMEPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA MAENEO YA POSTA – DAR ES SALAAM YENYE NO: **TAE 507295** ILIYOTOLEWA MAKAO MAKUU UHAMIAJI DAR ES SALAAM, MWAKA : 2022
TAARIFA YA UPOTEVU ILITOLEWA KATIKA KITUO CHA POLISI ILALA NA KUPEWA RB **NO : REF: PHQ/DAR/ILA/9086/2023**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**JOHN FERDINAND MLWILO**

Mtajwa hapo juu anatangaza kupotelewa na Passport (hati ya kusafiria) yenye namba AB656166 kwa atakae lona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu kwa **KUMB:RB:PHQ/MWA/ILE/1132/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DENIS P. MALLEY** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0168-0010** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SANU SEMINARY SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/CEN/RB/212561/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**FRED ELIHURUMA MOSHI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index number **S1098/537** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MAJI YA CHAI SEKONDARI** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/UBU/7546/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANDREW JAMES BROWNING** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 774 CUB** aina ya **TOYOTA HIACE** yenye CHASSIS NO. **IH1291007615.** ENGINE NO. **315050326.** Yeyote atayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi **PHQ/ARU/ARU/1545/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI**
**Mkoa D'SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na 1314…./2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SALUMU MOHAMED MKWAMA WA D'SALAAM**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA IBRAHIM SALUM MKWAMA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 25 mwezi 09 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

**Imetolewa leo Tarehe 4 Mwezi 9 Mwaka 2023**

HAKIMU

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BOSCO BERNARD MSUNGU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya BMW yenye usajili namba **T329 CBX ,** CHASSIS NAMBA: **WBAAM12070FN0248** na ENGINE NAMBA: **206SEAA2428.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/1564/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JULIUS MAMBOLEO LYIMO** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 284 CPN** aina ya **TOYOTA LANDCRUISER** yenye CHASSIS NO. **JTER871J500009555.** Yeyote atayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi **PHQ/ARU/ARU/1546/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**ROMAN FREDRICK METTA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 904 EDS TOYOTA HARRIER.** Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 394 BJV TOYOTA PRADO.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/8989/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**MROKI SHABANI IBRAHIM** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 596 BSX TVS KING** yenye Chassis namba **MD6M14PK7H4B65296.** Engine namba **OK4BH4385798**. Yeyote atayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi **ARU/ARU/RB/169349/2023.**

---

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM,MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## AZIMIO LA NAIROBI LIKISAINIWA;

# Juni, Julai, Agosti yavunja rekodi joto duniani

**Nairobi, KENYA**

WAKATI nchi za barani Afrika zikitarajia kusaini Azimio la Nairobi, kuhusu hali ya hewa, Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia hali ya hewa, limesema kwamba miezi mitatu iliyopita, ilikuwa na joto kali zaidi kuwahi kurekodiwa duniani.

Mazungumzo yaliyohitimishwa jana, mjini Nairobi, viongozi wa Afrika, wanatafuta azimio la pamoja kuangazia uwezo wa bara hilo wa matumizi ya nishati jadidifu.

Azimio hilo la Nairobi linanuia kuweka mfumo wa mwelekeo wa vitendo kukuza sekta ya nishati mbadala na kuongeza ufadhili wa ulinzi wa hali ya hewa kwa mataifa ya Afrika.

Maofisa wanasema, kulingana na takwimu, Afrika inahusika na ongezeko la viwango vya chini vya joto la chini ya asilimia nne, ingawa inalipa gharama ya kubwa kubwa kutokana na athari za joto.

Viongozi hao pia watatoa wito kwa mataifa yanayochangia zaidi utoaji wa hewa chafu, kutimiza ahadi zao za muda mrefu kuhusu hali ya hewa kwa mataifa maskini.

**JOTO KALI**

Shirika hilo limesema jana kwamba, kutokana na takwimu za Idara ya Umoja wa Ulaya inayojihusisha na masuala ya mabadiliko ya tabianchi la Copernicus Climate Change na kuongeza kuwa Agosti, ilivunja rekodi ya kuwa na joto kali zaidi.

Ulaya yakumbwa na matokeo mabaya ya hali ya hewa. Mwezi huo wa Agosti kulingana na shirika hilo ilipindukia wastani wa karibu nyuzi joto 1.5 za Celsius, ikilinganishwa na wakati wa kabla ya mapinduzi ya kiviwanda.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, ameonya juu ya kitisho dhahiri kitokanacho na mabadiliko ya tabianchi. **DW**



Wafanyakazi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), wakizibua chemba iliyokuwa imeziba na kutiririsha maji machafu katika barabara ya Uhuru, eneo la Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# ...Marais wawili wawasili

**Na Restuta James**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amesema wakuu wawili wameshawasili kwa ajili ya kuhudhuria mkutano wa marais katika Jukwaa la Kuimarisha Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF).

Vilevile, amesema askari wameongezwa huku baadhi ya barabara zikitarajiwa kufungwa, ili kuwawezesha wageni kuhudhuria bila usumbufu mkutano huo mkubwa barani Afrika.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Chalamila alisema tayari Rais wa Burundi, Evarist Ndayishimiye alikuwa ameshawasili, pia wa Senegal, Macky Sall.

"Na kesho asubuhi (leo) tunatarajia kuwapokea marais wengine wa Afrika Mashariki akiwamo Rais wa Kenya, William Ruto," alisema.

Mkuu wa Mkoa alisema wataendelea kutoa taarifa kadri viongozi hao wanavyowasili.

Kuhusu usalama na ratiba za njia, Chalamila alisema ulinzi umeimarishwa kwa kuongeza askari na kuweka utaratibu wa matumizi katika baadhi ya barabara hususani ya Nyerere, inayotumiwa na wageni wanaowasili.

"Ikilazimika tutafunga baadhi ya njia ili kuwahudumia vizuri wageni wetu, pia kuhakikisha wananchi wetu hawasumbuki," alisema.

**"Na kesho asubuhi (leo) tunatarajia kuwapokea marais wengine wa Afrika Mashariki akiwamo Rais wa Kenya, William Ruto," alisema.**

# Benki ya Dunia yaipa Tanzania bil. 740/- kilimo cha umwagiliaji

**Na Renatha Msungu**

BENKI ya Dunia (WB) imetoa mkopo wa Dola za Marekani milioni 300 (zaidi ya Sh. bilioni 746) kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima wadogo nchini.

Fedha hizo ambazo ni mkopo wa muda mrefu kwa serikali, zitatumika ndani ya miaka mitano kwa ajili ya utekelezaji shughuli za kilimo, ikiwamo uboreshaji wa miundombinu ya wakulima wadogo.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alibainisha hayo jana wakati wa uzinduzi wa Programu ya Mpango wa Kustahimili Mifumo ya Chakuka nchini, uliofanyika jana jijini Dar es Salaam pembeni mwa Kongamano la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF).

Alisema fedha zinakwenda kufanya kazi katika hekta 37,000 ambazo zimetengwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji ambacho vijana wengi wamejikita.

Bashe alisema kuwa kabla ya kutolewa kwa fedha hizo, walikaa kikao kujadili kuhusu matumizi yake.

"Tunaishukuru sana serikali kwa kuridhia mkopo huu kwenye sekta ya kilimo. Ninaamini zinakwenda kuleta matokeo chanya kwenye kilimo cha umwagiliaji na kulinufaisha taifa," alisema Bashe.

Kutokana na hilo, Waziri Bashe aliwataka Watanzania kujikita katika kilimo kama wanavyofanya katika suala la mazingira ili kuhakikisha kilimo kinakubalika kwa jamii. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar, Shamanta Shaame Khamis, alishukuru serikali kutokana na kuanzisha programu hiyo ambayo inakwenda kuwainua wakulima.

Alisema kwa upande wa Zanzibar, watakwenda kuboresha miundombinu mbalimbali ya kilimo ili kuhakikisha kilimo kinapiga hatua na kuwainua wakulima kiuchumi wao na familia zao.

Waziri huyo alimpongeza Bashe kutokana na kubuni mradi huo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali huku akisisitiza taifa linakwenda kuinuka kupitia kilimo.

Alisema mradi huo ni sehemu muhimu sana kwao kwa sababu wanakwenda kuwekeza katika miundombinu ya umwagiliaji katika hekta ambazo zimetengwa kwa ajili ya kilimo hicho.

Awali, akiwakaribisha wazungumzaji, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweri, alisema alipongeza AGRF kwa kushirikiana na serikali kuandaa mkutano huo ambao unakwenda kuleta manufaa makubwa kwa taifa na wakulima kwa ujumla.

Mweri alisema wakulima na wafanyabiashara wanapaswa kutumia fursa hiyo ambayo imetolewa na serikali kwa ajili ya kupiga hatua katika shughuli za kilimo wanazofanya.



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (katikati), akikata utepe kuzindua ofisi ya kuleta mapinduzi ya kilimo nchini (ATO), jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Biteko atoa maagizo 10 kukabili ndoa kuvunjika, watoto mitaani

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

NAIBU Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko, ametoa maelekezo mahsusi 10 kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum katika kudhibiti wimbi la watoto wa mitaani.

Pia, amemtaka waziri mwenye dhamana kushirikiana na vyombo vya sheria kushughulikia wamiliki wa makao ya watoto, vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na makazi ya wazee wanaovitumia kama vitega uchumi na kujinufaisha wenyewe.

Dk. Biteko ambaye ni Waziri wa Nishati, alitoa maelekezo hayo jana jijini hapa katika mkutano wa Maofisa Ustawi wa Jamii kwa niaba ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Alisema ustawi wa jamii ukifanya kazi vizuri kwa mipango, kutakuwa na ndoa imara na zile zenye migogoro zitatafutiwa suluhu kwa haraka na hivyo kupunguza wimbi la watoto wa mitaani kwa kuwa wengi ni zao la migogoro hiyo.

"Nimefahamishwa kwamba katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, jumla ya mashauri 28,773 yalipokewa na kati ya hayo, 22,844 yalifanyiwa usuluhishi katika Mabaraza ya Usuluhishi na Ofisi za Ustawi wa Jamii na 5,929 yalipewa rufani kwenda mahakamani," alisema.

Alibainisha kuwa migogoro ya ndoa kwa kipindi hicho ilipungua kwa asilimia 27 katika kipindi hicho kutokana na jitihada zinazoendelea kufanywa na wadau mbalimbali.

"Viongozi tusione jambo la ustawi wa jamii kama jambo dogo, ni jambo kubwa. Nenda katembelee vituo uone watoto wanaolelewa, hawajui baba zao wala mama zao, wanakula kwa misaada ya watu.

"Wapo ambao kwa sehemu kubwa wanabeba mzigo wa uhusiano wa watu. Ukiliona jambo hilo, vaa viatu vyao, wahurumie watoto hao na uiangalie Tanzania ya miaka 50 ya watoto wanaotokana na mazingira haya uone hatari iliyoko mbele yetu," alisema.

Naibu Waziri Mkuu aliagiza wizara kuendelea kuwatambua na kuwapatia huduma watoto walio katika mazingira hatarishi ikiwa ni pamoja na huduma za chakula, malazi, mavazi, elimu, matibabu na lishe.

"Watoto 335,971 walio katika mazingira hatarishi wametambuliwa na kupatiwa huduma katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023. Miongoni mwa hao, watoto 26,000 waliotelekezwa, manusura wa vitendo vya ukatili, waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu na wanaoishi kwenye makao ya watoto wameunganishwa na familia zao ili kuwahakikishia malezi, matunzo na ulinzi," alisema.

Dk. Biteko pia alikemea tabia ya baadhi ya wanaume kutelekeza familia zao na wengine kutowajibika kutunza watoto waliowazaa wenyewe.

Kuhusu wamiliki wa makao na vituo, Naibu Waziri Mkuu aliagiza wanaotumia kujinufaisha wachukuliwe hatua za kisheria na kutoa rai kwa watu wote na taasisi zinazotoa huduma za ustawi wa jamii katika vituo visivyosajiliwa, kuvisajili vituo hivyo ndani ya siku 90 kuanzia jana.

"Baada ya hapo, ukaguzi wa kina utafanyika ili kubaini watakaoshindwa kutimiza vigezo vya kisheria ili wachukuliwe hatua," alisema.

Kuhusu baadhi ya maelekezo mahsusi, aliagiza wizara hizo na wadau kuhakikisha mchakato wa mapitio ya Sheria ya Mtoto na kanuni zake ukamilike ili kuhakikisha watoto wanapata ulinzi na malezi stahiki.

"Wakurugenzi wa halmashauri watenge fedha kwa ajili ya huduma za ustawi wa jamii kwa mujibu wa mwongozo wa mipango, bajeti na taarifa za ustawi wa jamii, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma iendelee kutoa ajira kwa Maofisa Ustawi wa Jamii, kuimarisha programu ya huduma ya afya ya akili na msaada wa kisaikolojia ili kupunguza athari zinazotokea ndani ya familia na jamii,"aliagiza.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema katika mkutano huo kuwa umezinduliwa Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji, Usimamizi na Uratibu wa Mabaraza ya Usuluhishi wa Migogoro ya Ndoa Mwaka 2023.

Alisema kuwa pia kuna Mwongozo wa Mafunzo ya Uwiano wa Kijinsia na Ujumuishwaji Jamii katika Huduma za Ustawi wa Jamii 2022 na Kiongozi cha Taifa cha Uelimishaji wa Huduma za Ustawi wa Jamii na Majukumu ya Viongozi.

Alisema upungufu wa maofisa hao unatishia ustawi wa jamii.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, alisema wamekutana na migogoro mingi ya ndoa na wamekuwa wakifanya kazi kwa karibu na Maofisa Ustawi wa Jamii ili kusuluhisha kabla ya kupelekwa mahakamani.

"Migogoro hiyo kwa mujibu wa RITA inaongezeka na watoto wamekuwa wakiathirika zaidi. Takwimu za hivi karibuni za RITA zinaonesha kwamba, kati ya watoto milioni nne wanaoishi na kufanya kazi mitaani, zaidi ya asilimia 40 wanatoka kwenye familia zilizovunjika, hii ni changamoto kubwa kwa kizazi kijacho," alisema.

Mwenyekiti wa Maofisa Ustawi wa Jamii, Martin Chuwa, alisema kuna ongezeko la afya ya akili kwa wananchi, mmomonyoko wa maadili na wazazi na walezi kutotimiza wajibu wao, hali inayochangia kuwapo watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani.

"Kuna upungufu mkubwa wa maofisa hawa kwa asilimia 80 kwa ngazi ya kata na asilimia 60 ngazi ya halmashauri," alisema.

## KESI KINA MDEE

# Komu aihusisha NEC na wabunge 19

**Na Grace Gurisha**

MWENYEKITI wa Bodi ya Wadhamini wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Maulida Komu (73), amedai mahakamani kuwa taarifa ya Halima Mdee na wenzake 18 kughushi barua ya kuwa wabunge walishirikiana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) alizitoa kwenye kiapo kinzani ambacho hakukiandaa yeye.

Mdee na wenzake walifungua shauri namba 36/2022 Julai 22, 2022 wakiomba mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama na kisha itoe amri tatu.

Komu alidai hayo jana mbele ya Jaji Cyprian Mkeha wa Mahakama Kuu Masjala Kuu, Dar es Salaam wakati akijibu maswali ya dodoso kutoka kwa jopo la mawakili wa wabunge hao ambao ni Ipilinga Panya, Aliko Mwamanenge na Edson Kilatu.

Maswali hayo ya dodoso yanatokana na kiapo alichokiwasilisha mahakamani hapo, baada ya Mdee na wenzake 18 kufungua shauri hilo la kikatiba kwa kupinga kuvuliwa uanachama.

**Kilatu:** Kwenye kiapo chako umesema waleta maombi waliitwa na hawakwenda na pia umesema walishirikiana na NEC kughushi barua ya kuwa wabunge, lakini hapo awali umeieleza mahakama hukuwapo kwenye kikao cha baraza kuu, je, hizi taarifa ulizitoa wapi?

**Komu:** Taarifa hizi nilizipata baada ya kusoma kiapo kinzani ambacho sikuandika mimi na kuhusu kwamba hawakwenda niliambiwa walipewa nafasi ya kujitetea na hawakwenda kwa hiyo nisome halafu ni saini.

**Kilatu:** Kuna sehemu unawatuhumu Halima na wenzake kuwa walijiteua kuwa wabunge, habari hizo ulizitoa wapi wakati ulikuwa hushiriki vikao vya baraza kuu?

**Komu:** Nilipokwenda ofisini kwa katibu wa chama ndiyo nilielezwa hayo, kwasababu kama unataka kujua taarifa za chama unazipata huko.

Kilatu: Hapa mahakamani kuna kiapo kinzani kinachoonesha kimesainiwa na wajumbe saba ikiwamo wewe, je, unakitambua?

**Komu:** Ndiyo nakitambua

**Kilatu:** Uliapa mambo uliyokuwa unayajua kweli au si kweli?

**Komu:** Kweli

**Panya:** Chama kiliwaita kwa njia gani?

**Komu:** Waliandikiwa barua ya wito, lakini hawakufika kwasababu walisema ulinzi ulikuwa mdogo.

**Panya:** Halima na wenzake wanalalamika kuwa wamefukuzwa bila kuitwa?

**Komu:** Wao hawakutaka kusikilizwa, waliitwa na hawakwenda kwasababu ukikosana na mtu na akikuita lazima uende ili msuluhishane sasa wao waliitwa ila hawakwenda.

**Panya:** Umesema waliitwa na walikataa kwenda kwasababu ya kuhofia usalama wao, je, wewe unaona suala la usalama wao ni dogo?

**Komu:** Si dogo kama ni kweli.

**Panya:** Halima na wenzake wanadai waliomba wapewe siku saba ili walete utetezi wao kwasababu kulikuwa na shida ya usalama wao.

Komu: Sina habari kama waliomba au kuleta barua ya kuomba hizo siku saba.

**Panya:** Je, unawatambua waleta maombi kama walikuwa viongozi wa chama chako?

**Komu:** Natambua.

**Panya:** Je, ulishiriki kikao kilichofanyika Mei 11, 2022 kama mjumbe wa baraza kuu?

**Komu:** Hata sikuwapo kabisa kwasababu mimi sio mjumbe wa baraza kuu.

**Kilatu:** Moja ya malalamiko ni kwamba John Mnyika na Freeman Mbowe kuingia kwenye kikao cha kamati kuu na wakati walipoenda kukata rufani wakawakuta hao hao kwenye baraza kuu hivyo ni kinyume cha sheria na kanuni ya chama chenu, wewe unasemaje?

**Aliko:** Unamfahamu kama kuna taratibu za mtu kuvuliwa ubunge?

**Komu:** Ndio zipo taratibu

**Aliko:** Kama NEC ilishawatamka kuwa wabunge, je, Chama kilifuata taratibu za kupinga wasiwe wabunge?

**Komu:** Ndiyo kwa kuwa chama hakiwatambui.

**Aliko:** Hawa 19 kamati kuu iliwavua ubunge au uanachama?

**Komu:** Iliwavua uanachama.

Hakimu Mkeha aliahirisha shauri hilo hadi leo saa tatu asubuhi kwa ajili ya kuendelea na maswali ya dodoso.

Mdee na wenzake walifungua shauri hilo namba 36/2022 Julai 22, 2022 wakiomba Mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama na kisha itoe amri tatu.

Katika shauri hilo, wabunge hao wanaiomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama na pia iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kuwasikiliza.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MBAPPE KUTUA LIVERPOOL
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 24, anaripotiwa yuko tayari kwa wazo la kujiunga na Liverpool msimu ujao huku akitafuta njia ya kuondoka Paris St-Germain 2024. **(L'Equipe)**

### FERGUSON ANUKIA CITY
KLABU ya Manchester City inamfuatilia mshambuliaji wa Brighton, Evan Ferguson, mwenye umri wa miaka 18, ambaye ni raia wa Jamhuri ya Ireland na anaweza kucheza pamoja na Erling Haaland. **(inews)**

### WAN-BISSAKA MAMBO SAFI
MANCHESTER United wameanza kujadili mkataba wa beki, Aaron Wan-Bissaka baada ya kiwango cha nyota huyo mwenye umri wa miaka 25 kumvutia Kocha, Erik ten Hag mwaka huu. **(Telegraph)**

### FELIX ALIIKACHA LIVERPOOL
LIVERPOOL ilikuwa tayari kubadilishana mshambuliaji wa Uruguay, Darwin Nunez, mwenye umri wa miaka 24 na winga, Joao Felix (23), msimu huu, lakini mchezaji huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno aliwapuuza Wekundu hao.**(Mail)**

### UNITED HALI NGUMU
WAZABUNI wawili wakuu katika kinyang'anyiro cha kuinunua Manchester United wamesema hawajaambiwa kama klabu hiyo itaondolewa sokoni licha ya kushuka kwa bei ya hisa ya Mashetani Wekundu kwa pauni milioni 600. **(Mail)**

### STERLING BADO SANA
MSHAMBULIAJI wa Chelsea na England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 28, hatastaafu kucheza soka la kimataifa licha ya kuachwa tena kwenye kikosi cha England chini ya Kocha, Gareth Southgate. **(Telegraph)**

### GRAY KUONDOKA EVERTON
WINGA wa Everton na Jamaica, Demarai Gray (27), anatarajiwa kuondoka Goodison Park na kuingia mkataba wa miaka minne na klabu ya Al-Ettifaq ya Saudi Arabia ambayo inanolewa na gwiji wa zamani wa Liverpool, Steven Gerrard. **(Fabrizio Romano)**

### LINGARD AGOMBEWA ULAYA
KLABU ya West Ham imejiunga na Galatasaray na Fenerbahce katika kinyang'anyiro cha kuwania kumsajili kiungo wa zamani wa Manchester United na England, Jesse Lingard, mwenye umri wa miaka 30. **(Football Insider)**

### LINDSTROM ALIICHAGUA NAPOLI
KIUNGO wa Denmark, Jesper Lindstrom, mwenye umri wa miaka 23 alikataa uhamisho wa pauni milioni 25 kutoka Eintracht Frankfurt kwenda Liverpool na badala yake akajiunga na Napoli kwa sababu atapata muda zaidi wa kucheza na mabingwa hao wa Serie A. **(Tipsbladet)**

### MAATSEN KUBAKIA CHELSEA
CHELSEA inamtaka beki wa pembeni, Ian Maatsen, kukubali mkataba mpya wa muda mrefu pale Stamford Bridge baada ya Mholanzi huyo kukataa uhamisho wa pauni milioni 31 kwenda klabu yake ya zamani ya Burnley kwa mkopo siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la uhamisho **(Fabrizio Romano)**

### JORGINHO BADO YUPO
WAKALA wa Jorginho amesema kiungo huyo wa kati wa Italia mwenye umri wa miaka 31, atabakia Arsenal licha ya kutakiwa na Fenerbahce inayoshiriki Ligi Kuu Uturuki, ambapo dirisha la uhamisho litaendelea kuwa wazi hadi Septemba 15, mwaka huu. **(Tutto Mercato)**

---------------------------

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AL-ITTIHAD YAKOMAA KUMSAJILI MO SALAH

Hatima yake kujulikana leo jioni wakati dirisha la usajili...

**LIVERPOOL, England**

KLABU ya Al-Ittihad haijakata tamaa katika kujaribu kupata sahihi ya mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, kabla ya saa ya mwisho ya kufungwa kwa pazia la usajili, kwa mujibu wa 90min.

Pazia la dirisha la usajili la Saudi Arabia linafungwa rasmi leo na Al-Ittihad wanaamini wanaweza kukamilisha usajili wake kabla ya kufungwa kwa dirisha hilo.

Salah amekuwa mlengwa mkubwa wa soka la Saudi Arabia kwa muda mrefu, lakini mipango ya awali ya kumsajili ilikwama baada ya Liverpool kukataa ofa mbili kutoka kwa klabu hiyo.

Raia huyo wa Misri mwenye umri wa miaka 31 alipoulizwa kuwa nahodha ajaye wa Liverpool baada ya nahodha wa zamani, Jordan Henderson kuondoka kuelekea Al-Ettifaq Julai na baadhi ya marafiki wa karibu wa Salah katika mchezo huo wamekosoa waziwazi jinsi mchezaji huyo anavyochukuliwa na bosi wa Wekundu hao, Jurgen Klopp.

Klopp mara kwa mara aliweka msimamo wake wazi hataki kumpoteza nyota huyo kutoka Kaskazini mwa Afrika.

90min ilifichua mapema msimu huu wa joto Mfuko wa Uwekezaji wa Umma wa Saudi Arabia (PIF) - wamiliki wa Al-Ittihad wanawania kumsajili Salah.

Ofa ya maneno ya pauni milioni 150 ilikataliwa mwezi uliopita na Liverpool, lakini Al-Ittihad wanakataa kurejea tena mezani na wako tayari kuvunja rekodi ya dunia ya uhamisho ya pauni milioni 200 kwa Salah.

Kuna mipango ya kumfanya awe mwanasoka bora wa kulipwa duniani, kushinda hata mkataba wa sasa ambao Cristiano Ronaldo anayecheza katika klabu Al Nassr.

Tarehe ya mwisho ya uhamisho wa Ligi ya Saudia itafikia tamati leo jioni. Licha ya kuwa zimesalia saa chache, Al-Ittihad wanaendelea kushinikiza kumsaka Salah.


Wanaamini kabisa anataka kuhama na kitu pekee kinachosimama kwenye njia ya makubaliano ni makubaliano na wamiliki wa Liverpool.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,151,10

MECHI KALI
ALGERIA
VERSUS
TANZANIA
1 | 1.39
X | 3.96
2 | 9.25

# VINICIUS JR APAMBANA KURUDI DIMBANI HARAKA




**MADRID, Hispania**

VINICIUS Junior anafanya bidii binafsi kuharakisha kupona kutoka kwenye jeraha la misuli ya paja na kurejea uwanjani kabla ya muda uliopangwa.

Fowadi huyo wa Brazil aliumia katikati ya kipindi cha kwanza cha ushindi wa 1-0 dhidi ya Celta Vigo Agosti 25, mwaka huu na akalazimika kuwa nje ya dimba baada ya vipimo kuthibitisha alikuwa ameumia msuli wake wa paja la kulia.

Alitarajiwa kukosa kucheza kwa angalau wiki sita, lakini gazeti la Marca limesema kuna matumaini yanayoongezeka huko Madrid, Vinicius anaweza kurejea haraka kuliko ilivyotarajiwa.

Madaktari wa klabu wanafahamika kuona mechi ya dabi ya Madrid dhidi ya Atletico, ambayo imepangwa kuchezwa Septemba 24, mwaka huu kama tarehe ya kweli ya kurudi kwa Vinicius.

Uchunguzi umefanywa kila siku tangu Vinicius alipoondoka uwanjani kwa mara ya kwanza na wanaohusika wanasema maendeleo yake ni mazuri.

Jeraha hilo liliongeza kile ambacho kimekuwa mwanzo mgumu kwa kampeni ya sasa ya Vinicius, ambaye alikuwa akizoea maisha katika jukumu jipya uwanjani.

Kuondoka kwa Karim Benzema na baadaye kusajiliwa kwa kiungo Jude Bellingham kumemfanya Kocha, Carlo Ancelotti kuachana na mfumo wa 4-3-3 ambao ulifanya maajabu kwa Vinicius na kupendelea 4-1-2-1-2 ili kuongeza mchango kwa raia huyo wa England.

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Musa Samweli - 0653 711 XXX
2. Sudick Saad - 0658 239 XXX
3. Abdallah Lindonde - 0673 125 XXX
4. Mkombozi Nyamya - 0676 135 XXX
5. Fortinatus Mhonda - 0678 543 XXX
6. Benandi Mwakasege - 0711 997 XXX
7. Abdallah Mohammed - 0713 304 XXX
8. Fredy Fredy - 0717 215 XXX
9. Leonard Ngugi - 0718 997 XXX
10. Nasibu Ramadhani - 0719 348 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# Van Gaal: Argentina ilibebwa

**AMSTERDAM, Uholanzi**

LOUIS van Gaal amedokeza matokeo ya Kombe la Dunia la FIFA mwaka jana nchini Qatar "yalitengenezwa" ili kumsaidia Lionel Messi hatimaye kubeba kombe hilo akiwa na Argentina.

Messi aliiongoza Argentina kunyakua ubingwa wake wa kwanza na watatu wa Kombe la Dunia kwa nchi yake mnamo Desemba, mwaka jana, nyota huyo alipofunga mara mbili kwenye fainali na kusaidia taifa hilo la Amerika Kusini kuishinda Ufaransa kwa penalti 4-2 kwenye Uwanja wa Lusail.

Awali Argentina walikuwa wameiondoa Uholanzi nje ya michuano hiyo katika hatua ya robo fainali baada ya kuwafunga kwa penalti kufuatia sare ya mabao 2-2.

Van Gaal, ambaye alijiuzulu kama Kocha Mkuu wa Uholanzi baada ya kuondoka kwenye Kombe la Dunia, alisema alifikiri mchezo wao dhidi ya Argentina ulikuwa wa kupangwa.

"Sitaki kusema mengi kuhusu hilo," alisema Van Gaal akiwaambia waandishi wa habari.

"Unapoona jinsi Argentina walivyofunga mabao yao na jinsi tulivyofunga mabao yetu, na jinsi baadhi ya wachezaji wa Argentina walivyovuka alama na hawakuadhibiwa, basi nadhani wote ulikuwa mchezo wa kupangwa."

Alipoulizwa kufafanua alichomaanisha, Van Gaal alisema: "Namaanisha kila ninachosema."



## HABARI MICHEZO

04,636/-

# MWAKINYO, OKWIRI ULINGONI SEPTEMBA 29

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Hassan Mwakinyo, anatarajia kupanda ulingoni kupigana na Mkenya, Rayton Okwiri, katika pambano la kuwania mkanda wa ubingwa wa IBA.

Pambano hilo linatarajia kufanyika Septemba 29, mwaka huu kwenye ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, promota wa pambano hilo, Ali Mndeme, alisema tayari makubaliano ya kuandaa pambano hilo kati ya IBA na Mwakinyo yamefikia katika hatua nzuri.

Mndeme alisema wanatarajia pambano hilo litakuwa na ushindani kutokana na ubora wa mabondia wanaokutana.

"Litakuwa pambano la kuwania mkanda wa kimataifa, tumejipanga vizuri safari hii moto utawaka, kwa sababu mbali na pambano hilo ambalo litakuwa kubwa, pia tutakuwa na mapambano ya utangulizi makali," alisema Mndeme.

Aliongeza Mwakinyo anaendelea vyema na mazoezi ya kujiandaa na pambano hilo na amejipanga kupeperusha vizuri bendera ya Tanzania.

"Kila kitu kinakwenda vizuri, tunatarajia kuwa na pambano lenye hadhi ya kimataifa, kila bondia atakayepanda ulingoni ataonyesha ubora wake, tunawaomba wadau wa mchezo wa ngumi waje kupata burudani,' aliongeza promota huyo.



Msanii wa muziki wa kizazi kipya, Rubi, akitumbuiza katika Mkutano wa Kimataifa wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika unaofanyika jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba SC, Yanga katika hesabu kali

INATOKA UK. 24

inzani wao kupitia mikanda ya video na kuamua kubadilisha programu zake kwa lengo la kuwaongezea utimamu wa kutosha wachezaji wake kabla ya mchezo huo.

Mmoja wa viongozi wa timu hiyo katika benchi la ufundi ambaye hakutaka jina lake litajwe alisema mwalimu baada ya kuangalia mikanda ya wapinzani wake kuna kitu alikibaini na kuamua kuongeza dozi hiyo ya mazoezi.

"Unajua mwalimu alitoa mapumziko wikiendi na ndiyo maana Jumatatu tulianzia ufukweni kwa ajili ya wachezaji kurudisha utimamu wao kabla ya kurejea uwanjani kuendelea na ratiba zengine za kiufundi, amebaini wapinzani wetu wana nguvu hivyo ameamua pia kuwaongezea stamina wachezaji wetu" alisema kiongozi huyo.

Alisema Gamondi na benchi lake la ufundi wanajua wanachokitaka baada ya kuwangalia wapinzani, hali iliyomlazimu kubadilisha programu kwa kuongeza muda zaidi wa kufanya mazoezi kulingana na ukubwa wa mchezo uliopo mbele yao kwa sasa.

Alisema Yanga imepania kutinga hatua ya makundi na ndio sababu wanapanga mikakati yao vizuri na kuwasoma wapinzani wao kabla ya kukutana katika mechi mbili zitakazoamua timu yao kusonga mbele.

Michezo ya marudiano ambayo itafanyika jijini Dar es salaam inatarajiwa kuchezwa kati ya Septemba 29 na 30 mwaka huu.

## Taifa Stars pointi 1

INATOKA UK. 24

Tayari timu 15 zimefuzu kucheza fainali hizo mpaka sasa akiwemo mwenyeji Ivory Coast, timu nyingine ni pamoja na Guinea, Equatorial Guinea, Algeria, Burkina Faso, Cape Verde, Misri, Guinea-Bisau, Mali, Morocco, Nigeria, Senegal, Afrika Kusini, Tunisia na Zambia.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.09/09/23 | 17:00 | AFC Wimbledon vs Stockport County FC | 2.75 | 3.20 | 2.47 |
| 02.09/09/23 | 17:00 | Milton Keynes Dons vs Notts County | 2.60 | 3.55 | 2.41 |
| 03.09/09/23 | 17:00 | Accrington Stanley vs Mansfield Town | 2.95 | 3.40 | 2.24 |
| 04.09/09/23 | 17:00 | Crawley Town vs Newport County | 3.00 | 3.30 | 2.25 |
| 05.09/09/23 | 17:15 | Burgos CF vs SD Eibar | 2.80 | 2.90 | 2.65 |
| 06.09/09/23 | 19:30 | Real Oviedo vs Sporting Gijon | 2.25 | 2.90 | 3.40 |
| 07.09/09/23 | 20:45 | Cobh Ramblers vs Athlone Town AFC | 2.36 | 3.40 | 2.48 |
| 08.09/09/23 | 22:30 | Virgin Islands, British vs Turks and Caicos Islands | 2.44 | 3.30 | 2.45 |
| 09.10/09/23 | 00:00 | Cerro Largo FC vs CA Fenix Montevideo | 2.46 | 3.00 | 2.60 |
| 10.10/09/23 | 03:30 | FC Tulsa vs Phoenix Rising FC | 2.41 | 3.25 | 2.50 |
| 11.10/09/23 | 04:00 | Colorado Springs Switchbacks FC vs San Antonio FC | 2.60 | 3.25 | 2.34 |
| 12.10/09/23 | 05:30 | Portland Timbers vs Los Angeles FC | 2.65 | 3.50 | 2.19 |
| 13.10/09/23 | 14:30 | Shanghai Jiading City Dev vs Heilongjiang Ice City | 2.60 | 3.15 | 2.40 |
| 14.10/09/23 | 16:00 | Kazakhstan vs Northern Ireland | 2.55 | 2.90 | 2.60 |
| 15.10/09/23 | 16:00 | CA Cerro vs CA River Plate (URU) | 2.42 | 2.95 | 2.70 |
| 16.10/09/23 | 19:00 | Faroe Islands vs Moldova | 2.80 | 2.90 | 2.40 |
| 17.10/09/23 | 21:00 | Tristan Suarez vs Deportivo Riestra | 2.75 | 3.00 | 2.60 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 07/09/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 4175 | Iraq vs India | 1.46 | 3.77 | 6.73 |
| 15:00 | 1986 | Karlsruher SC vs SC Freiburg | 5.00 | 3.90 | 1.50 |
| 15:00 | 3255 | Cambodia vs Hong Kong | 5.19 | 4.07 | 1.61 |
| 15:00 | 5864 | Nurnberg vs Heidenheim | 3.10 | 3.65 | 1.91 |
| 16:00 | 4277 | Northern Ireland U21 vs Luxembourg U21 | 1.27 | 5.10 | 8.36 |
| 16:30 | 4561 | Belarus U21 vs Faroe Islands U21 | 1.68 | 3.62 | 4.38 |
| 16:30 | 4877 | Thailand vs Lebanon | 1.44 | 3.98 | 6.53 |
| 17:00 | 3765 | Kazakhstan vs Finland | 3.58 | 3.27 | 2.11 |
| 17:00 | 5427 | Flamengo RJ U20 vs Palmeiras SP U20 | 2.39 | 3.30 | 2.64 |
| 17:30 | 2001 | Estonia U21 vs Bulgaria U21 | 5.10 | 4.08 | 1.52 |
| 18:00 | 1029 | Ringsted IF vs HB Koge | 10.03 | 6.34 | 1.19 |
| 18:15 | 3635 | Qatar vs Kenya | 1.70 | 3.71 | 4.98 |
| 18:45 | 3909 | Hungary U21 vs Kazakhstan U21 | 1.25 | 5.29 | 8.95 |
| 19:00 | 2396 | Ghana vs Central African Republic | 1.36 | 4.16 | 9.56 |
| 19:00 | 2888 | Aalesund 2 vs Brattvag | 2.21 | 3.83 | 2.52 |
| 19:00 | 3039 | Bulgaria vs Iran | 3.91 | 3.33 | 1.99 |
| 19:00 | 3101 | Lithuania vs Montenegro | 5.06 | 3.48 | 1.74 |
| 19:00 | 4004 | Angola vs Madagascar | 1.48 | 3.90 | 6.86 |
| 19:00 | 4602 | San Marino U21 vs Norway U21 | 40.73 | 9.78 | 1.03 |
| 19:00 | 4825 | Czech Republic U21 vs Slovakia U21 | 1.80 | 3.46 | 3.92 |
| 19:00 | 5170 | Staal Jorpeland vs Vidar | 3.73 | 4.34 | 1.63 |
| 19:00 | 5437 | Egypt U23 vs Russia | 2.90 | 3.21 | 2.48 |
| 19:30 | 2398 | Hapoel Kfar Saba vs Hapoel Afula | 2.26 | 3.06 | 3.22 |
| 19:30 | 2538 | Maccabi Herzliya vs Sectzya Nes Ziona | 3.55 | 3.00 | 1.98 |
| 19:30 | 2813 | Ironi Tiberias vs Ironi Hasharon | 1.90 | 3.10 | 3.65 |
| 19:30 | 3465 | Hapoel Nir Ramat Hasharon W vs Hapoel Petach-Tikva W | 5.20 | 5.00 | 1.37 |
| 19:30 | 4314 | El Fahem vs Hapoel Acre | 2.17 | 2.90 | 3.15 |
| 19:30 | 4342 | SC Kfar Qasem vs Hapoel Rishon Lezion | 2.52 | 2.95 | 2.90 |
| 19:30 | 5593 | France U21 vs Denmark U21 | 1.67 | 3.56 | 4.57 |
| 19:45 | 1484 | Bosnia and Herzegovina U21 vs Slovenia U21 | 2.13 | 3.25 | 3.10 |
| 20:00 | 1077 | Norway vs Jordan | 1.36 | 4.86 | 8.25 |
| 20:00 | 2899 | Cyprus U21 vs Austria U21 | 5.52 | 4.19 | 1.47 |
| 20:30 | 1558 | Bnot Netanya W vs AS Tel Aviv University W | 4.08 | 4.59 | 1.57 |
| 21:00 | 2291 | Caxias RS vs Ferroviario CE | 2.15 | 3.01 | 3.31 |
| 21:00 | 2754 | Alianza Universidad De Huanuco vs Los Chankas CYC | 1.86 | 3.52 | 3.47 |
| 21:30 | 1286 | Alcorcon vs Rayo Vallecano | 4.90 | 3.70 | 1.55 |
| 21:30 | 4856 | Austria vs Moldova | 1.12 | 8.05 | 22.24 |
| 21:45 | 2225 | Netherlands vs Greece | 1.53 | 4.08 | 6.17 |
| 21:45 | 2911 | Denmark vs San Marino | 1.06 | 10.35 | 52.78 |
| 21:45 | 3500 | France vs Ireland | 1.29 | 5.20 | 10.59 |
| 21:45 | 3941 | Czech Republic vs Albania | 1.59 | 3.75 | 6.13 |
| 21:45 | 4576 | Wales vs South Korea | 2.48 | 3.43 | 2.74 |
| 21:45 | 4580 | Poland vs Faroe Islands | 1.20 | 6.11 | 15.74 |
| 21:45 | 4824 | Serbia vs Hungary | 1.76 | 3.54 | 4.75 |
| 21:45 | 5181 | Slovenia vs Northern Ireland | 1.85 | 3.39 | 4.45 |
| 22:00 | 2349 | Niger vs Uganda | 3.32 | 2.96 | 2.27 |
| 22:00 | 3618 | Algeria vs Tanzania | 1.39 | 3.96 | 9.25 |
| 22:00 | 4772 | Municipal Turrialba vs Guadelupe FC | 3.10 | 3.46 | 2.05 |
| 22:20 | 5294 | Ferroviaria SP W vs Corinthians W | 4.38 | 3.57 | 1.69 |
| 23:00 | 1059 | Anguilla vs Saint-Martin | 2.16 | 3.47 | 2.86 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Alhamisi Septemba 7, 2023

Nipashe




**Al-Ittihad yakomaa kumsajili Mo Salah** UKURASA 21



Baadhi ya wachezaji wa Timu ya Taifa ,'Taifa Stars' wakiwa katika mazoezi kabla ya kukabiliana na Algeria kwenye mchezo wao wa kwanza kuwania kufuzu fainali za Afrika uliochezwa Juni 8 mwaka jana, Uwanja wa Benjamini Mkapa. Stars ilifungwa mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# TAIFA STARS POINTI MOJA TU LEO ALGERIA

## ●●●Itakuwa imejihakikishia kufuzu fainali za Afrika kwa mara ya tatu hata kama...

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya soka ya Tanzania, Taifa Stars leo itakuwa na kazi moja tu ya kusaka angalau pointi moja ili kuweka rekodi ya kucheza Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) kwa mara ya tatu katika historia ya nchi itakaposhuka dimbani kucheza dhidi ya Algeria, huku Serikali ikiitakia kila la kheri.

Stars itashuka kwenye Uwanja wa Mei 19 uliopo kwenye mji wa Annaba Kaskazini mwa nchi hiyo majira ya saa 4:00 kwa saa za Afrika Mashariki, ikijaribu kurudia ilichokifanya mwaka 1979 na 2018 ilipofuzu kucheza AFCON ambazo fainali zake zilichezwa 1980 nchini Nigeria na 2019 nchini Misri.

Ofisa Habari wa Mawasiliano wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), Cliford Ndimbo amesema kikosi kimejiandaa vyema kwani kiliwasili salama jana kutoka mjini Tabarka nchini Tunisia na kilifanya mazoezi mepesi kwa ajili ya pambano hilo, huku kikiwa na wachezaji wote, isipokuwa nahodha wa timu hiyo, Mbwana Samatta ambaye alitarajiwa kuwasili baadaye tayari kwa pambano hilo.

"Kikosi kimeshajiandaa na kiko tayari kwa mchezo huo, nia ya wachezaji, benchi la ufundi, Serikali na TFF ni kuhakikisha tunacheza fainali za AFCON kwa mara nyingine tena," alisema Ndimbo.

Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma amesema mchezo wa leo una umuhimu mkubwa na wa kipekee kwa sababu Stars inahitaji pointi moja tu iweze kufuzu bila kuangalia matokeo ya mechi nyingine.

"Mchezo huu una umuhimu mkubwa sana ukilinganisha na mingine mingi ambayo tumecheza katika miezi kadhaa huko nyuma kwa sababu sasa tunahitaji pointi moja bila kuangalia matokeo ya mechi nyingine, lakini pengine tunaweza kupata sare na Uganda tukawa tumefuzu moja kwa moja," alisema.

Stars inayohitaji ushindi au sare ipo kwenye Kundi F, ambalo linahitaji timu moja kuungana na Algeria ambayo tayari imefuzu kucheza fainali hizo.

Msimamo wa kundi hilo kabla ya michezo ya leo, Algeria anaongoza akiwa na pointi 15 akifuatiwa na Taifa Stars wenye pointi saba huku Uganda wakishika nafasi ya tatu wakiwa na pointi nne huku Niger ikiburuza mkia.

Kutokana na msimamo huo, Stars hata ikipata sare itakuwa imefuzu moja kwa moja fainali hizo zitakazochezwa Ivory Coast hata kama Uganda itafanikiwa kuifunga Niger.

INAENDELEA UK. 23

# Simba SC, Yanga katika hesabu kali

**Faustine Feliciane na Saada Akida**

KLABU za Simba na Yanga zipo kwenye mahesabu makali kuhakikisha wanapata ushindi mzuri kwenye michezo yao ijayo ya Ligi ya mabingwa Afrika huku kila kocha akiweka wazi mipango yake kuelekea kwenye mechi hizo.

Wakati Simba itasafiri mpaka Zambia kuumana na Power Dynamos ya nchini humo Septemba 16 kuwania kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo, Yanga wenyewe watasafiri kwenda Rwanda kuifuata Al Merrikh ambao wamechagua kucheza mchezo wao wa nyumbani nchini humo Septemba 17.

Kocha wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' amesema kwa sasa wachezaji wake wameonyesha wapo tayari kwa mechi kubwa za kimataifa kutokana na uwezo wanaouonyesha mazoezini na mechi mbili za kirafiki walizozicheza zimempa mwanga.

Alisema anafahamu ugumu watakaoupata kutoka kwa wapinzani wao hao lakini hana hofu yoyote kutokana na maandalizi anayoendelea kuyafanya.

"Kwa sasa akili zetu zipo kwenye mchezo dhidi ya Power Dynamos, kitu kizuri kwangu ni viwango vya wachezaji wangu, wameimarika zaidi na kila mmoja anaonyesha utayari wake, ili ni jambo zuri kwangu kuelekea kwenye mchezo huu," alisema Robertinho.

Alisema baada ya kumalizana na Wazambia hao ndipo ataanza kupanga mikakati yake kuelekea kwenye michuano ya 'Africa Football League' ambapo wamepangwa kucheza na mabingwa wa Misri, Al Ahly.

Wakati Robertinho akisema hivyo kwa upande wa Simba, Kocha wa Mabingwa wa soka nchini, Yanga, Miguel Gamondi mwenyewe ameanza kufungua faili lake la mbinu kali kuelekea katika mchezo wao dhidi ya Al-Merrikh ya Sudan kuwania kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo.

Gamondi ameendelea kuwaongezea dozi ya mazoezi wachezaji wake ambapo kwa sasa wanafanya mara mbili kwa siku.

Taarifa za uhakika kutoka ndani ya Yanga zilizoifikia Nipashe jana, zinaeleza benchi la ufundi chini ya kocha huyo limefanya tathmini kubwa kuelekea katika mchezo huo baada ya kuwasoma wap-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >